# UWAZI NA UMAANISHO: USIMBAJI MAANA KIMAZUNGUMZO KATIKA EKEGUSII NA KISWAHILI

**NA**

**OCHICHI ALICE KERUBO**

**C50/68927/2011**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

**2013**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote

____________________________ ______________

OCHICHI ALICE KERUBO TAREHE

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimanizi wa kazi hii tulioteuliwa na chuo kikuu.

____________________________ ______________

PROF. J. H. HABWE TAREHE

____________________________ ______________

DKT. J. N. MICHIRA TAREHE

## SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati ninamtolea Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia uhai, mali, ujuzi na nguvu zilizoniwezesha kuikamilisha kazi hii.

Ninawashuru sana wazazi wangu Yuvenalis Ochichi na Pacifica Mosomi ambao walinilea na kunielimisha. Ni kwa juhudi na mapenzi yao nilipata msingi mzuri wa masomo ambao umeniwezesha kufika hapa nilipofika.

Ninawashukuru sana wasimamizi wangu Prof. Habwe na Dkt. Michira kwa kuchukua muda wao licha ya shughuli nyingi walizokuwa nazo, na kuipitia kazi yangu na kisha kunielekeza vilivyo. Maarifa yao, mapendekezo ya kitaalam pamoja na mawaidha ya kiusomi waliyonipa ndiyo yameifanikisha kazi hii.. Ninamshukuru sana Prof. Habwe kwa kunifundisha somo la semantiki na pragmatiki ambalo ndilo kiini cha sanaa ya kiusemi. Uwazi na ukarimu wake wa kimawazo ulinifaa sana katika kuikamilisha kazi hii. Dkt Michira, maelekezo ya kiujuzi aliyonipa yameninoa vilivyo licha ya mapungufu mengi niliyokuwa nayo mwanzoni, ninashukuru sana kwa kuniwezesha kukamilisha kazi hii.

Ninawashukuru sana wahadhiri wote wa Idara ya Isimu na Lugha katika Chuo Kikuu cha Nairobi ambao walinifundisha. Ni kupitia kwa mafunzo, ushauri na kututia moyo kwao nilipata ari ya kukamilisha masomo yangu. Wahadhiri hao ni pamoja na Prof. Kithaka wa Mberia, Prof. Abdulaziz, Prof. Wamitila, Prof. Habwe, Dkt Kineene wa Mutiso, Dkt Buregeya, Bw. Mungania, Dkt Mbatiah, Dkt. Mukhwana, Dkt. Zaja na Dkt. Olali.

Wenzangu tulioanza safari hii pamoja sitawasahau kwa mengi tuliyofanya pamoja, joto la ushirika, kuhimizana pamoja na mijadala tuliyofanya pamoja ambayo imetuwezesha kuufikia ufanisi huu. Marafiki wa karibu ambao ni pamoja na Jedidah Mwangi, Janepher Murumba, na Elizabeth Yego, ahsante sana. Wenzangu wa somo la Isimu ni pamoja na Rahab, Zipporah, George, Kennedy, Thobias, Janet, Rose, Mary, Tobias, Beatrice, Keziah, Margaret na Pauline nawashukuru sana.

Shukrani zangu za pekee ni kwa familia yangu, na hasa mume wangu mpendwa John Kennedy Nyambane kwa uvumilivu wake nilipokuwa mbali na nyumbani, pamoja na kujitwika mzigo wa kuikimu familia yetu katika muda wote wa masomo yangu. Zaidi ya yote, alimvumilia mke aliyekuwa na msongo wa kimawazo. Watoto wangu Martin, Esther, Jared na Deborah, siku nyingi walikosa uwepo na mapenzi ya mama; naye Susan tuliyeishi naye katika kipindi chote cha masomo yangu, asanteni sana kwa subira yenu.

Ninawashukuru jamaa wengine ambao walichangia pakubwa kufanikisha kazi yangu. Shangazi Josephine wa Mjini Kisii aliyenisaidia katika ukusanyaji wa data, nasema ahsante sana. Sitamsahau mwandani wangu Rebecca Moraa ambaye nilifanya mashauriano naye kila wakati katika kutafuta fafanuzi zaidi kuhusu kategoria za kimuktadha. Dadangu Irene Nyambeki, simu alizonipigia ziliniinua, nilipokuwa chini, nasema asante sana. Rafiki wa karibu Sam Njoroge, nashukuru kwa maneno yako yaliyonitia moyo kila wakati. Mkoi wangu Bathsheba, asante kwa mengi tuliyoshiriki pamoja. Shiroh ambaye aliichapisha kazi yangu kwa uangalifu na subira, nawashukuru sana na wengine wote ambao walinisaidia kwa njia moja au nyingine, na ambao sijaweza kuwataja, nasema asante sana.

## TABARUKU

Ninaitabaruku tasnifu hii kwa

Wanangu wapendwa;

Martin

Esther

Jared na

Deborah

Mna kila sababu ya kufaulu.

Kwa wanafunzi wangu,

Mtu habaki vilevile siku zote!

## YALIYOMO

IKIRARI ........ ii
SHUKRANI ........ iii
TABARUKU ........ v
ISTILAHI ZILIZOTUMIKA ........ ix
IKISIRI ........ x

SURA YA KWANZA ........ 1
MSINGI WA UTAFITI ........ 1
1.1 Utangulizi ........ 1
  1.1.1 Lugha ya Kiswahili ........ 3
  1.1.2 Lugha ya Ekegusii ........ 4
1.2 Tatizo la Utafiti ........ 5
1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 6
1.4 Nadharia Tete ........ 7
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ........ 7
1.6 Upeo na Mipaka ........ 9
1.7 Misingi ya Nadharia ........ 10
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 13
  1.8.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Lugha ya Kiswahili ........ 13
  1.8.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Lugha ya Ekegusii ........ 15
  1.8.3 Yaliyoandikwa katika Pragmatiki ........ 17
1.9 Mbinu za Utafiti ........ 19
  1.9.1 Ukusanyaji wa Data ........ 20
  1.9.2 Watoa Habari ........ 20
  1.9.3 Hojaji ........ 20
  1.9.4 Uwasilishaji wa data na uchanganuzi wake ........ 20

SURA YA PILI ....................................................................................................21
KATEGORIA ZA KISEMANTIKI ...........................................................................21
2.1 Utangulizi .....................................................................................................21
2.2 Kategoria za Kileksika...................................................................................22
2.3 Kategoria za Kimuktadha ..............................................................................27
2.4 Uainishaji wa Kategoria za Kimuktadha ........................................................30
2.4.1 Mbinu za Lugha na Tamathali za Semi ......................................................31
2.4.2 Methali.......................................................................................................31
2.4.3 Nahau.........................................................................................................32
2.4.4 Tashibihi ....................................................................................................34
2.4.5 Taashira......................................................................................................35
2.4.6 Sitiari..........................................................................................................36
2.5 Hitimisho .......................................................................................................37

SURA YA TATU ................................................................................................38
KATEGORIA ZA KISEMANTIKI ZA KISWAHILI NA EKEGUSII..............38
3.1 Utangulizi .....................................................................................................38
3.2 Kategoria za Kisemantiki za Kiswahili .........................................................40
3.2.1 Nomino za Kiswahili..................................................................................41
3.2.2 Vitenzi vya Kiswahili .................................................................................43
3.3 Kategoria za Kisemantiki za Ekegusii...........................................................45
3.3.1 Nomino za Ekegusii....................................................................................46
3.3.2 Vitenzi vya Ekegusii...................................................................................48
3.4 Kategoria za Kimuktadha za Kiswahili na Ekegusii .......................................52
3.4.1 Methali za Kiswahili na za Ekegusii .........................................................53
3.4.2 Nahau.........................................................................................................61
3.4.3 Nahau za Kiswahili.....................................................................................63
3.4.4 Nahau za Ekegusii ......................................................................................65
3.4.5 Tamathali za Usemi ....................................................................................69

3.4.6 Tashibihi ........................................................................................69
3.4.7 Taashira..........................................................................................71
3.4.8 Sitiari...............................................................................................73
3.5 Hitimisho ..........................................................................................74

SURA YA NNE..........................................................................................76
MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..................................................76
4.1 Utangulizi ..........................................................................................76
4.2 Mahitimisho........................................................................................76
4.3 Mapendekezo......................................................................................81

MAREJELEO.............................................................................................82
KIAMBATISHO ........................................................................................87
HOJAJI ......................................................................................................87

## ISTILAHI ZILIZOTUMIKA

| | |
|---|---|
| Uwazi | (Explicature) kinachomaanishwa na kauli kutokana na maana za msamiati uliotumiwa. |
| Umaanisho | (Implicature) kile kinachomaanishwa na msemaji wa kauli ingawa hakidhihiriki kutokana na maneno yaliyotumiwa. |
| Pragmatiki | Taaluma ya isimu inayochunguza maana ya neno kimatumizi, kimuktadha, kimazingira, kiwakati na kiutamaduni. |
| Sheria ya Dahl | Ilipewa hilo jina na Carl Meinhof (1903). Mwasisi wake ni Edmund Dahl. Inahusu silabi mbili sughuma zinapofuatana moja huwa ghuna k.v. mkate – mgate (Kishambala), tatu – datu (Kinyamwezi), Kikuyu – Gikuyu. kitabu – egetabu (Ekegusii) |
| Kategoria za kisemantiki | (Semantic domains) Jinsi lugha hugawa maneno kulingana na matumizi ya maneno hayo. |
| Kategoria za kimuktadha | (Contextual semantic domains) tamathali za usemi. |
| Kategoria tambuzi | (Cognitive categories) uanishaji wa maneno katika lugha kwa mujibu wa sifa za maneno hayo. |
| Kiunzi cha ufahamu | (Cognitive frame) Sehemu kwenye kauli palipo na msisitizo. |
| Maneno makuu | (Content words) Maneno yanayobeba jumbe muhimu katika lugha. |
| Maneno ya kimatumizi | (Functional words) Maneno yanayoambatanishwa na maneno makuu kukamilisha tungo. |
| Fasiri ya kimaarifa | (encyclopaedic interpretation) ujuzi unaotumiwa kufikiria maana inayofaa katika kauli fulani. |

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza jinsi wazungumzaji hutumia misimbo inayozua uwazi na umaanisho katika lugha za Kiswahili na Ekegusii kwa lengo la kubainisha kama kuna mlingano wowote kati ya lugha hizi, zote zikiwa lugha za Kibantu. Lugha hizo zimeelezwa kisemantiki ambapo maana msingi za kauli zimechanganuliwa, na baadaye maana za kipragmatiki kuelezwa kwa kutumia Nadharia ya Uhusiano. Nadharia ya Uhusiano ya Sperber na Wilson (1986) ilitumiwa kufasiri misimbo iliyotokana na kategoria mbalimbali za lugha hizi mbili ambapo kanuni za uhusiano pamoja na kanuni ya ujuzi wa msikilizaji zilisaidia kupata fasiri iliyokusudiwa na wasemaji wa kauli mbalimbali.

Tasnifu hii ina sura nne. Katika sura ya kwanza, tumeshughulikia utangulizi kwa jumla. Tumeeleza kuhusu lugha za Kiswahili na Ekegusii, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchangua mada, upeo na mipaka misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada yetu pamoja na mbinu za utafiti tulizotumia.

Katika sura ya pili, tumejadili kuhusu kategoria za kisemantiki kwa jumla ambapo tumebainisha makundi mawili makuu ya kisemantiki ambayo ni pamoja na kategoria za kileksika na kategoria za kimuktadha.

Sura ya tatu imejadili kategoria mbalimbali za kisemanti ambazo huibuka kimazungumzo katika lugha ya Kiswahili na vilevile lugha ya Ekegusii na kueleza uwazi na umaanisho wa kauli hizo. Ufafanuzi wa maana kiumaanisho umefanywa kwa kutumia mbinu za kinadharia za uhusiano. Nadharia ya Uhusiano ilitumiwa ambapo ilibainika kwamba lugha hizi mbili zinatumia mitindo tofauti kuzua umaanisho. Aidha, tofauti za kiuteuzi wa maneno zimebainishwa katika lugha zote. Sababu za tofauti hizo zimejadiliwa.

Katika sura ya nne, mahitimisho na mapendekezo yametolewa ambazo nadharia tete pamoja na madhumuni ya utafiti yametathminiwa. Kutokana na tathmini hizo pamoja na uchanganizi wa data yetu, tumerejelea nadharia tete zetu ambapo baadhi zimekubaliwa na nyingine kukanushwa. Vilevile, katika sura hii tumetoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

Uchanganuzi wa misimbo mbalimbali ulidhihirisha tofauti za uteuzi wa kategoria za kisemantiki zinazotumika katika lugha za Kiswahili na Ekegusii, na maana zilizosimbwa pia zilibainisha tofauti kadha wa kadha. Hali hii ilibainishwa na tofauti za fahamu za awali za tamaduni katika lugha hizo mbili, mitazamo pamoja na mazingira ya watumizi wa lugha hizi.

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Mazungumzo ndiyo njia kuu ya mawasiliano inayotumika katika muktadha wa kijamii. Mazungumzo ni yale matumizi ya lugha kati ya watu katika hali mahususi na huongozwa na uwezo na mitazamo wa wazungumzaji. Vipengele vikuu vinavyoongoza mazungumzo ni uhalisia pamoja na hali ya kiakili. Sauti huwa ni za kiuhalisia kwa vile zinasikika ilhali maana zinazobebwa na sauti hizo hueleweka kiakili. Mazungumzo hutokea miongoni mwa watu katika mitagusano na shughuli zao za kila siku. Mara nyingi, mazungumzo hayo hutumikiza mbinu zisizo za moja kwa moja ili kupitisha ujumbe. Mbinu hizo za usimbaji maana pamoja na miktadha husaidia kujenga na kufanikisha ufaafu wa jumbe zinazokusudiwa. Mazungumzo ya kijamii ni suala ambalo halijazingatiwa sana kiutafiti katika lugha hizi ingawa linadhihirisha umaanisho mwingi katika kauli zenye fasiri za uwazi, (Ullman, 1970).

Uwazi na umaanisho hubainika katika lugha nyingi. Uwazi ni maana ya kileksika ya tamko kwa lengo la kupitisha ujumbe. Maana kiuwazi hutokana na maana za kidhahania za msamiati uliotumiwa kwenye kauli. Maana huibuka kutokana na taratibu na mpangilio wa maneno kutoka kwa mtoaji hadi kwa mpokezi wa ujumbe. Maneno yote katika lugha fulani yana maana za kidhahania ambayo kimatumizi huzua uwazi. Umaanisho ni maana ya kauli kimuktadha na kile

msemaji anamaanisha ingawa hajakisema. Fasiri ya kauli hutokea kama umaanisho wakati wahusika katika mazungumzo wanaufikia ujumbe ulionuiwa na mtoaji katika kauli ingawa ujumbe wenyewe haudhihiriki kileksika. (Levinson, 1983; Leech, 1983; Yule, 1996).

Lugha za Ekegusii na Kiswahili ni lugha za Kibantu. Lugha za Kibantu ni ambishi. Lugha hizi huambatisha vambishi kwenye mizizi ya maneno ili kuunda maneno mapya. Viambishi hivyo hubeba maana za njeo, idadi, nafsi, hali, kauli, ukanushaji na ngeli (Polome, 1967; Guthrie, 1970; Massamba, 2004). Maneno ya lugha za Kibantu hufuata muundo wa konsonanti, vokali, konsonanti na vokali. Lugha hizi zina matumizi mengi ya umaanisho katika mazungumzo kwenye miktadha mahususi. Kategoria mahususi za kisemantiki zinapotumiwa katika miktadha fulani kimazungumzo huzua umaanisho. Utata huwa unazuka iwapo miktadha ya matumizi ya kategoria fulani za kisemantiki haibainiki. Matumizi ya lugha kimazungumzo hubainisha uwazi na umaanisho katika miktadha mbalimbali. Kwa kutumia Nadharia ya Uhusiano, utafiti huu ulibainisha maana za baadhi ya kategoria za kisemantiki katika lugha ya Ekegusii na kuilinganisha na zile za Kiswahili ili kuonyesha iwapo kuna mshabaha wowote wa matumizi ya kategoria za kisemantiki katika miktadha ya kijamii mnamotumika lugha hizi.

Tofauti moja kubwa inayobainika kati ya lugha za Kiswahili na Ekegusii ni ile ya kisauti ambapo katika lugha ya Ekegusii, sauti ambayo sighuna huwa ghuna

inapofuatwa na sauti nyingine sighuna kulingana na sheria ya Dahl. Sifa hii hubainika katika lugha za Kibantu za Kaskazini Mashariki. Sifa hii haibainiki katika lugha ya Kiswahili. (Bickmore, 1998). Katika lugha ya Ekegusii pia toni inaweza kuzua umaanisho kwa vile ina jukumu muhimu sana kama kipengele cha muundo wa lugha hii kinyume na lugha ya Kiswahili.

### 1.1.1 Lugha ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kibantu ambayo chimbuko lake ni upwa wa Afrika Mashariki. Lugha hii iliainishwa na Guthrie (1948) kama lugha ya Kibantu ya kundi la G. Kiswahili kina lahaja nyingi. Lahaja zilizobainishwa na Guthrie (1948) ni kumi na nane. Lugha hii ni lingua franka na inazungumzwa na watu wengi katika maeneo mengi tofautitofauti ya Afrika Mashariki, Afrika ya Kati na Kusini. Aidha, inazungumzwa katika eneo la kusini mwa Oman kule Uajemi (Polome, 1967; Mbaabu, 1991; Chimerah, 1998).

Kiswahili ni lugha ya kitaifa na pia lugha rasmi nchini Kenya na Tanzania. Katika sera za lugha za nchi hizi mbili, Kiswahili kimejumuishwa kama somo rasmi katika mitalaa ya elimu na hivyo kinafundishwa kuanzia shule za msingi, za upili, pamoja na vyuo vikuu. Pia lugha hii hutahiniwa katika mitihani ya kitaifa katika shule za msingi na za upili katika nchi za Afrika Mashariki. (Iribemwangi na Mukhwana 2011).

Lugha ya Kiswahili inatambuliwa kama lugha ya kimataifa kwa sababu inatumika katika shughuli za kiuchumi, kidini na kisiasa katika ngazi za kimataifa. Vyuo vingi barani Afrika, Ulaya, Asia na Marekani vinafundisha somo la Kiswahili. Vituo vingi vya redio hurusha matangazo yao kwa lugha ya Kiswahili pia. Kiswahili ni miongoni mwa lugha zilizotafitiwa sana na kuandikiwa vitabu vingi na makamusi. Maandishi mengi ya Kiswahili yamechapishwa na kusambazwa yakiwemo majarida, vitabu vya dini, riwaya, tamthilia, mashairi na nyimbo zinazoimbwa pamoja na vitabu vya hadithi fupi. Kazi nyingi pia zimetafsiriwa kwa Kiswahili. Wazungumzaji wa Kiswahili wanakadiriwa kuwa zaidi ya watu milioni 140, (Chimerah 1998; Lewis na wenzake 2013) katika makala ya Ethnologue Toleo la 17.

### 1.1.2 Lugha ya Ekegusii

Lugha ya Ekegusii, kama lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Lugha hii inazungumzwa katika kaunti za Kisii na Nyamira ambazo ziko kusini magharibi mwa nchi ya Kenya. Miji mikuu ya kaunti hizi ni Kisii na Nyamira mtawalia. Guthrie (1948) ameainisha lugha ya Ekegusii kama lugha ya Kibantu ya kati ambayo iko kundi moja na lugha ya Kikuria katika kundi la E.42. Lugha hii inahusishwa na lugha ya Lagooli, Kikuria na Kimeru za Kenya, Ware, Ikisu, Ikoma na Sanjo zote za Tanzania.

Jamii ya Abagusii imezingirwa na jamii nyingine ambazo si jamii-lugha moja nayo. Upande wa magharibi imepakana na jamii ya Waluo na upande wa kaskazini imepakana na jamii ya Wakipsigis. Imepakana na Wamaasai upande wa kusini. Asili ya Abagusii ni eneo lililo kati ya Nigeria mashariki na Cameroon. Baadaye walihamia Congo kabla ya kuingia nchini Kenya kutoka upande wa magharibi na kutulia katika milima ya Gusii (Kapiyo na wenzake 1996).

Idadi ya Abagusii ni zaidi ya watu milioni 2.2 ambao ni asilimia kumi ya jumla ya watu nchini Kenya kuambatana na takwimu za sensa ya (2009).Jamii hii ina watu wengi mno mashambani nchini Kenya ikilinganishwa na maeneo mengine.Kuna watu takriban 500 katika kila kilomita mraba. Asilimia kubwa ya Abagusii ni wanauwili-lugha kwa maana kuwa watu wengi wa jamii hii wanazungumza zaidi ya lugha moja. Takwimu za SIL (2009) zinaonyesha kwamba Ekegusii pia huzungumzwa nchini Tanzania katika eneo la Mara na Mkoa wa Serengeti, mtaa wa Kyambahi. Jamii ya Abagusii wanaipenda na kujivunia lugha yao.

**1.2 Tatizo la Utafiti**

Lugha yoyote inapotumika kimazungumzo huwa inaonekana kutumia misimbo ambayo huwa na maana fiche. Uchukuliaji wa juujuu wa maana za kauli zinazotokea katika mazungumzo hauwezi kutoa maana iliyokusudiwa. Aghalabu uelewa wa maana hujikita katika miktadha ya kijamii. Ni kutokana na hali hiyo utafiti huu ulipania kuchunguza jinsi usimbaji wa maana hutumika ili kuzua

umaanisho katika lugha za Kiswahili na Ekegusii. Aidha, miktadha ya kijamii panapotumiwa misimbo ilichunguzwa ili kubainisha kama kuna mlingano wowote kati ya lugha za Kiswahili na Ekegusii, zote zikiwa lugha za Kibantu.

Baadhi ya tafiti zilizofanywa katika Pragmatiki hasa zile zilizochunguza uwazi na umaanisho katika lugha mahususi zililenga miktadha tofauti na muktadha unaolengwa na utafiti huu, ukiwemo ule wa Kabiru (2012), na Ngoge (2012). Hakuna utafiti linganishi uliofanywa kubainisha tofauti za umaanisho unaozuka kimazungumzo katika lugha za Ekegusii na Kiswahili.

**1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Madhumuni ya utafiti huu ni kama yafuatayo:

i) Kubainisha baadhi ya kategoria za kisemantiki zinazotumiwa kusimba maana katika lugha za Kiswahili na Ekegusii.

ii) Kueleza baadhi ya misimbo inayozua umaanisho katika lugha ya Kiswahli na Ekegusii.

iii) Kufafanua miktadha ya matumizi ya misimbo inayo zua umaanisho katika lugha za Kiswahili na Ekegusii.

iv) Kuona ni vipi Nadharia ya Uhusiano inaweza kueleza maswala ya misimbo.

## 1.4 Nadharia Tete

Kuambatana na madhumuni ya utafiti huu, nadharia tete zifuatazo ziliibuka

i) Kategoria za kisemantiki zinazotumiwa kusimba maana katika lugha ya Kiswahili na Ekegusii zinafanana.

ii) Umaanisho wa misimbo katika lugha za Kiswahili na Ekegusii una ulinganifu mkubwa.

iii) Miktadha ya matumizi ya misimbo yenye umaanisho katika lugha ya Kiswahili na Ekegusii inafanana.

iv) Nadharia ya uhusiano inaweza kueleza swala la misimbo katika lugha hizi mbili.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Katika mazungumzo, maneno huwa yanaonekana kama yaliyo na na nguvu fulani ya kimiujiza. Uwezo huu wa maneno kubadilikabadilika kimaana kutoka kwa maana zake za kimsingi mara tu miktadha inapobadilika ndiyo imetupa motisha ya kufanya utafiti huu ili kubainisha jinsi maneno au vifungu vya maneno kwenye kauli husimba maana nyinginezo zenye uwazi na umaanisho katika mazungumzo ya kijamii katika lugha za Ekegusii na Kiswahili. Uchanganuzi wa mazungumzo ni suala muhimu sana kwani ni kupitia kwa mazungumzo lugha hutumiwa kiuhalisia kwenye mitagusano ya mara kwa mara kati ya wanajamii. Miundo ya kisanaa ya lugha pamoja na ufahamu wa kimawasiliano hudhihirika zaidi kiusemi na watumizi-lugha. Kila neno katika lugha fulani lina maana ya kidhahania

inayoeleweka na watumiaji wa lugha hiyo. Hata hivyo, maana msingi za maneno zinaonekana kubadilika maneno hayo yanapotumika kimazungumzo. Tofauti hizo za kimaana haziwezi kuelezwa kwa misingi ya kimofolojia, kisintaksia au kisemantiki (Wilson, 1967; Djik, 1985; Aichison, 2003; Habwe na wenzake, 2011).

Sababu ya kufanya utafiti huu ilikuwa kuchunguza iwapo kuna uhusiano wowote kati ya misimbo yenye umaanisho katika lugha ya Kiswahili na Ekegusii katika kuelezea dhana moja, ikikumbukwa kwamba lugha hizi mbili ni za Kibantu. Lengo kuu lilikuwa kuzilinganisha lugha hizi mbili kwa kubainisha jinsi wazungumzaji wake hutumia baadhi ya kategoria za kisemantiki kuzua umaanisho. Kigezo cha ulinganishi kinaupa utafiti huu upekee wake kwa kuwa tafiti nyingine zilitumikiza vigezo tofauti na hivyo kujaza pengo la ulinganishi wa lugha ya kiswahili na Ekegusii kwa kuchunguza jinsi misimbo hutumiwa kuzua uwazi na umaanisho.

Sababu nyingine ya kufanya utafiti huu ni kuchunguza kama Nadharia ya Uhusiano ingeweza kutumika kueleza jinsi fasiri sahihi zinafikiwa katika kauli zenye uwazi na umaanisho katika mazungumzo. Mazungumzo ni suala la kijamii (Macdonell, 1986). Kauli inapotolewa na msemaji, kuna maneno yanayotumika na maana za maneno hayo hutegemea ni wapi na ni kwa lengo gani yametumika. Neno lile lile au tamathali ile ile ya usemi inaweza kuibua maana mbili tofauti,

moja ikiegemea ukubalifu na nyingine ikiegemea hali ya ukinzani. Hivyo basi, uchunguzi wa kinadharia ungeweza kupima kama uhusiano utaweza kuziba pengo kati ya uwazi na umaanisho kimazungumzo. Upimaji huu wa kinadharia ulifanywa kwa kulinganisha lugha mbili, shughuli ambayo haijafanywa na tafiti nyingine za awali.

### 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulichunguza maana za kileksika na za kipragmatiki katika lugha za Ekegusii na Kiswahili. Aidha, ulishughulikia zaidi kauli za kimazungumzo jinsi huwa zinabainika katika miktadha ya kijamii. Jamii inachukuliwa hapa kama jumla ya mtu mmoja mmoja, na watu hao, kila mmoja katika upekee wake, huchangia katika kuiunda jamii. Watu hao wanaunganishwa na sifa nyingi zinazofanana katika kila mmoja wao, na kila mmoja kuendelea kukiri na kukubali sifa hizo za pamoja. Sifa hizo zinarejelewa kama 'makubalilano ya kawaida' (Mekacha, 2011). Shughuli hii ya kiulinganishi haikuingilia sana uchanganuzi wa kifonolojia, kimofolojia au kisintaksia ila tu wakati data husika ingehitaji hivyo.

Miktadha ambayo kwayo tulitoa mifano ya sentensi kimazungumzo ilikuwa ya kijamii ambapo watu hutangamana katika shughuli za kazi, sherehe mbalimbali pamoja na mazungumzo yanayolenga kukejeli, kujulisha, kushauri pamoja na kutoa maoni, na uwazi na umaanisho wa kauli hizo. Ni muhimu kutaja kwamba

lahaja ya Ekegusii tuliyotumia ni lahaja ya Rogoro inayotumika kama lahaja rasmi.Vilevile tulitumia Kiswahili sanifu katika utafiti huu.

**1.7 Misingi ya Nadharia**

Nadharia iliyotuongoza katika utafiti huu ni ile ya Sperber na Wilson (2002). Nadharia hii iliasisiwa 1986 kama wanavyoeleza Sperber na Wilson (2002) na kukua kwa hatua mbalimbali. Mihimili yake mikuu ni zile sifa ya mawasiliano ya binadamu, mawasiliano ya unenaji pamoja na yale ya ishara ambayo yanaeleza pamoja na kutambulisha makusudio ya utamkaji au usemi. Madhumuni ya Nadharia ya Uhusiano ni kueleza jinsi mpokezi wa kauli huifahamu maana ya msemaji kutokana na vidokezo anavyotoa yule msemaji pamoja na muktadha wa usemaji. Tamko lenyewe huzua matarajio yanayomwelekeza mpokezi wa kauli kwenye maana ilivyokusudiwa na msemaji.

Nadharia ya Uhusiano ina kanuni mbili kuu. Kanuni ya kwanza ni kanuni ya ufahamu wa ufaafu ambayo inapendekeza kwamba uwezo wa binadamu wa kiufahamu huelekezwa katika uzingatiaji wa uhusiano, na uwezo huu umeratibiwa ili kuzingatia mahusiano kwenye jumbe muhimu pekee. Kanuni ya pili ni ile ya kimawasiliano inayolenga ufaafu wa ujumbe unaopitishwa.

Wananadharia wa uhusiano wanaamini kwamba mawasiliano hutawaliwa na kanuni ya uhusiano, na kwamba makini ya msikilizaji hulenga tu zile jumbe zilizo

muhimu kwake, na hali hii inawezeshwa kwa kuhusisha jumbe hizo na jumbe za awali alizo nazo msemaji, ambazo anazihusisha na miktadha ya mazungumzo ya ya wakati mahususi ili kufikia ufaafu. Uhusiano unalenga kuteka makini ya msikilizaji na kuufanya ujumbe unaopitishwa kuwa muhimu kwake. (Sperber & Wilson, 2004). Tazama mfano ufuatao:

1. *Tata inche n'omonto omogima*


   Baba mimi ni mtu mzima

Kauli kama hii inapotolewa na kijana kwa baba yake katika mazungumzo ina ujumbe muhimu inaopitisha, kwamba kijana anaomba kupewa nafasi ya kujiamulia mambo yake, na kwamba hatarajii kuthibitiwa kila wakati.Ufahamu huu umejengwa kwenye misingi kwamba mtu mzima ana uhuru wa kujiamulia yale anayotaka kufanya.

Viwango vya uhusiano huelekezwa na kuongozwa na athari za miktadha pamoja na uwezo wa kiutendakazi wa kiufasiri. Miktadha inavyokuwa na athari zenye vidokezi vingi kuhusiana na ujumbe unaowasilishwa kwa msikilizaji, ndivyo ujumbe unavyokuwa na ufaafu zaidi. Iwapo msikilizaji atatatizika kuufikia ufasiri wa ujumbe muhimu uliomo kwenye kauli, hiyo inamaanisha kwamba ufaafu haujaafikiwa.Hivyo basi, ni muhimu kwa msikilizaji kujaribu awezavyo kuupa ujumbe fasiri mwafaka zaidi, yaani kutumia juhudi kidogo zaidi iwezekanavyo ili kupata ujumbe katika tamko. Uhusiano hujaribu kuitendesha kazi kanuni mojawapo ya Grice inayosema kwamba mawasiliano miongoni mwa watu, yawe

ya kiusemi au yasiyo ya kiusemi ni kule kufahamu na kutambua kusudi la kuwasiliana, ambalo huelekezwa na kule kupata manufaa  kwa msemaji dhidi ya msikilizaji katika shughuli nzima ya mawasiliano. (Thomas, 1995).

Ufafanuzi wa mbinu hii ya mawasiliano kimazungumzo inaweza kuonyeshwa kwa kielelezo kifuatacho:




Uwazi ni dhana katika taaluma ya pragmatiki inayoshughulikia maana ya tamko katika muktadha mahususi. Uwazi wa kauli ni kile kinachomaanisha kutokana na fasiri ya maana msingi ya maneno yaliyotumiwa. Uwazi ni kinyume na kile msemaji hukusudia lakini ambacho hakukisema. Thamani ya ukweli wa kauli hueleweka kutokana na uwazi wake kwa mfano.

2. *Mwane bachiire sobo*

   Kwangu wameenda kwao

Kauli ‘*mwane bachiire sobo’* ikifasiriwa moja kwa moja inamaanisha kwamba kuna watu wanaoitwa ‘*mwane*’ ambao wameenda kwao. Huu ndio uwazi wa tamko hili.

Umaanisho ni kile alichonuia mtoaji wa tamko hilo lakini hakidhihiriki katika maneno aliyotumia. Kauli iliyo na maneno ‘*mwane*’ na ‘*bachiire*’ yaliyotumika yamesimba maana ya ‘mke’ na ‘watu wengi walioenda’ mtawalia. Uwazi ni maana kileksika za misamiati katika sentensi ilhali umaanisho unajumlisha maana za kimakusudi za msemaji. Thamani kamili ya kauli hueleweka kwa kutambua muktadha kamili wa mazungumzo ili kuondoa utata, kupata ufahamu na kuelewa kauli za viwango ili kupata vitovu vya mambo yanayozungumziwa (Grice, 1975).

## 1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Katika sehemu hii tutajadili yaliyoandikwa kuhusu lugha za Kiswahili na Ekegusiii pamoja na yale yaliyotafitiwa katika taaluma ya pragmatiki, na hasa yale yanayolenga lugha mahususi ili kuchangia pia katika taaluma hii ya isimu.

### 1.8.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Lugha ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha za Kiafrika zilizofanyiwa utafiti mwingi sana. Kuna ithibati nyingi zinazoeleza mengi tangu chimbuko na historia

ya lugha hii, maendeleo yake, jinsi ilivyosambaa, hadhi yake katika ngazi za kataifa na za kimataifa pamoja na majukumu inayotekeleza kama lugha ya mawasiliano mapana. (Mbaabu, 1991; Chimerah, 1998). Sarufi ya lugha ya Kiswahili pia haijaachwa nyuma kiutafiti kutokana na wingi wa vitabu vilivyoandikwa, majarida, kazi za sanaa, vitabu vya kiada na vya ziada vinavyotumika kufundishia mashuleni na vyuoni pamoja na makamusi ya Kiswahili -Kiswahili na Kiswahili na lugha zingine.

Kuna makamusi mengi yaliyoandikwa na ambayo yanaeleza maana msingi za dhana mbalimbali katika lugha ya Kiswahili, mbali na yale makamusi yanayoeleza maana za tamadhali za lugha kama zinavyotumiwa na wazungumzaji wa lugha hii. Baadhi ya makamusi ya kimsingi tutakayotumia katika utafiti wetu ni TUKI (1990) na (2006) pamoja na Oxford (2004).

Tafiti katika sarufi na muundo wa lugha ya Kiswahili zimejumlishwa na wanaisimu wa Kiswahili kama vile Ashton (1947), Polome (1967), Mgullu (1999) pamoja na Habwe na Karanja (2004). Makala ya waandishi hao ndiyo yatakuwa kama mihimili ya ulinganishi wa kategoria za kileksika ambazo lugha hii itaweza kupimwa iwapo kuna mshabaha wowote na lugha ya Ekegusii, hasa zinapotumiwa kimazungumzo.

Kategoria za kimuktadha pia zimetafitiwa sana katika lugha ya Kiswahili. Kategoria za kimuktadha zinarejelewa kama tamathali za usemi ambazo ni pamoja na semi, nahau, istiari, methali, mafumbo, vitendawili, tashibihi, milio pamoja na mishangao miongoni mwa nyingine. Tamathali za lugha zinapotumika katika mazungumzo ya kawaida hubainika kama kategoria za kimuktadha, (Ottenheimer, 2006). Miktadha ya matumizi ya kategoria hizi katika lugha ya Kiswahili ndiyo pia itasaidia kufanya ulinganishi na ile inayotumika katika lugha ya Ekegusiii. Baadhi ya kazi zinazoratibu kategoria za kimuktadha ni ile ya Farsi (1973) Kuhenga (1977), Wamitilia (2001, 2003) na Arege & Nyanje (2011).

### 1.8.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Lugha ya Ekegusii

Kazi za kina zilizobainisha muundo wa lugha ya Ekegusii zimeeleza vijenzi pamoja na sifa mbalimbali za lugha hii. Kategoria za kisarufi pia zimeshughulikiwa kwa kiasi kikubwa kwa kuzingatia chukulizi za sifa za lugha za Kibantu. Uainishaji wa lugha za kibantu ulifanywa na Guthrie (1948). Lugha za Ekegusii na Kiswahili zilibainishwa kama lugha za Kibantu Kiswahili kikiwekwa katika kundi la G huku Ekegusii kikiwekwa katika kundi la E. Lugha hizi ndizo tunazolinganisha ili kubainisha kama kuna mlingano mkubwa wa kimuundo.

Gesare (1992) alitafiti mofolojia ya Ekegusii ambapo alionyesha kuwa maneno katika lugha hii yanaweza kutenganishwa kwa vipashio vyake na kila kipashio kikawa na maana mahususi. Utafiti huu unatoa mchango hasa katika uchanganuzi

wa maana za vitenzi vya lugha ya Ekegusii. Katika utafiti wetu unashughulikia jinsi baadhi ya maneno husimba maana na kuzua umaanisho.

Basweti (2005) alifanya uchanganuzi wa kimofosintaksi wa nomino wa elementi za sentensi ya Ekegusii. Utafiti hu ulipania kuchunguza muundo wa kimofolojia na kintaksia. Ni msingi mzuri wa kipragmatiki kwa vile vijenzi vya kimofosintaksi vinatumiwa na wazungumzaji vilevile kusimba maana zenye umaanisho.

Otiso (2008) alichanganua vitenzi vya Ekegusii kwa kutumia nadharia ya uminimalisti. Alionyesha kwamba katika mofolojia ya Ekegusii vitenzi huongezewa viambishi awali na viambishi tamati ili kuonyesha hali na njeo za vitenzi. Utafiti huu ni muhimu kwa kuwa tumerejelea baadhi ya vitenzi vya Ekegusii vinavyozua umaanisho kimazungumzo.

Tafiti hizi ni baadhi ya zile ambazo zimetoa maelezo jinsi lugha ya Ekegusii inavyoratibu vijenzi vyake kuunda maana katika viwango vya maneno, na utafiti wetu utayachunguza baadhi ya maneno hayo kimazungumzo na jinsi yanavyozua umaanisho kinyume na uwazi ambao ndio chukulizi msingi ya kimofolojia na kisemantiki.

### 1.8.3 Yaliyoandikwa katika Pragmatiki

Pragmatiki inahusu maana inayosimbwa kwenye kauli. Usimbaji maana ni kule kuficha maana kwa kutumia neno au fungu la maneno lenye maana zaidi ya fasiri ya kileksika ya maneno hayo. Fasiri inayotokana na neno au fungu hilo ndiyo umanisho kimazungumzo, ambapo lugha inadhihirika kiuamilifu.

Tafiti nyingi ambazo zimefanywa katika pragmatiki na ambazo zililenga lugha mahususi zilichunguza ama semantiki pekee au umaanisho pekee. Lengo kuu kama walivyopendekeza watafiti ni kueleza kategoria mahususi za lugha hizo. Waliobainisha maana msingi za kategoria za kileksika ni pamoja na Mwebia (2006) aliyetafiti kuhusu lugha ya Kimeru, Anyim (2010) alitafiti kuhusu lugha ya Dholuo na Omoke (2010) aliyetafiti kuhusu lugha ya Ekegusii. Watafiti hao walitumia Nadharia ya Semantiki Fahiwa. Utafiti wetu unanuia kuchunguza maana zinazozuka kimazungumzo, na ambazo ni tofauti na maana msingi za maneno hayo hayo kwa kutumia Nadharia ya Uhusiano ili kuziba pengo kati ya uwazi na umaanisho.

Tafiti za Warambo (2012) na Kabiru (2012) zilishughulikia miktadha na kategoria tofauti pia ikizingatiwa kwamba malengo ya kuzua misamiati mipya katika matumizi ya Sheng' katika kazi ya Warambo (2012) pamoja na Kabiru (2012) katika mizaha ni uwazi na umaanisho. Utafiti wetu utafanya ulinganishi wa lugha

mbili tofauti ili kuona jinsi uwazi na umaanisho hufasiriwa katika miktadha ya jamii mbili tofauti.

Chukulizi zisizo sahihi zinaweza kuzua umaanisho hasa miongoni mwa watu wanaotoka katika tamaduni na mazingira tofauti, na umaanisho wenyewe ukatukia kuwa sio ule uliokusudiwa. Hali hii ni kweli, hasa ikizingatiwa kwamba kategoria za kimuktadha hutofautiana kutoka kwa jamii moja hadi nyingine (Ogola, 2006). Hata hivyo chukulizi kama hizo zinaweza kuzuka miongoni mwa watu wanaozungumza lugha moja na kushiriki utamaduni mmoja kutokana na tofauti za umri, tofauti za mitazamo pamoja na ukosefu wa tajiriba katika matumizi ya misimbo hiyo inayozua umaanisho kinyume na uwazi. Suala hili ndilo utafiti huu unakusudia kufafanua, kwa kubainisha miktadha ya matumizi ya kategoria mahususi na uwazi na umaanisho unaozuka kwa kutumia Nadharia ya Uhusiano.

Katika utafiti wa Kimani (2008) uliotumia Nadharia ya Masharti Ukweli anaeleza kwamba masharti ukweli huibuka katika hali halisi. Anaeleza kuwa taaluma ya pragmatiki huzingatia maana, na maana ni lazima izingatie masharti ukweli. Ukweli usiobainika huwa unajazwa na mantiki. Mantiki hii ndiyo utafiti huu unakusudia kujaza kwa kueleza jinsi maana husimbwa kwenye uwazi na umaanisho kimazungumzo. Utafiti huo ulipendekeza tafiti zaidi kuhusu sifa za lugha ambazo hazizingatii kaida kama vile tamathali za lugha pamoja na mashairi yaliyo na umaanisho mwingi kiusemi.

Utafiti uliofanywa na Ngoge (2012) kuhusiana na umaanisho, anadokeza kwamba nahau hurutubisha lugha kimazungumzo. Nahau, kama kategoria ya kimuktadha pekee, mara nyingi huambatanishwa na kategoria zingine za kileksika ambazo huwa hazina maana funge kimazungumzo na ambazo zinaweza kuzua umaanisho vilevile. Mabadiliko ya miktadha ni suala ambalo husababisha mabadiliko ya maana za kategoria za kileksika ambazo zinaweza kukamilisha miktadha mnamotumika nahau, na hilo ndilo kusudi la utafiti huu.

Watumiaji wa lugha nyingi wanapozungumza huzua uwazi na umaanisho kwa pamoja. Kuziba pengo kati ya uwazi na umaanisho unaotokana na usimbaji maana kimazungumzo ni shughuli muhimu itakayofanywa na utafiti ambao utaonyesha mbinu mbadala ya fasiri za maana zilizoko kati ya uwazi na umaanisho, na kisha kuzihusisha kwa kufuata zile kanuni za uhusiano. Fasiri sahihi za uwazi na umaanisho uliosimbwa kwenye maneno na tamathali za usemi katika mazungumzo utaondoa utata kwa kuonyesha jinsi lugha ilivyo bunifu kiuamilifu kinyume na jinsi ilivyo kikaida.

**1.9 Mbinu za Utafiti**

Katika sehemu hii tulitoa maelezo kuhusu zile njia tutakazotumia katika utafiti huu.

### 1.9.1 Ukusanyaji wa Data

Njia ya kwanza tuliyotumia kukusanya data ni kutumia ujuzi wa mtafiti ambayo lugha yake asilia ni Ekegusii. Hata hivyo kulifanywa mashauriano na wazungumzaji wengine wa lugha hii ili kupata ufafanuzi zaidi. Kuhusiana na lugha ya Kiswahili, njia kuu tuliyotumia ni kusoma na kurejerea vitabu pamoja na makamusi ya Kiswahili ili kupata maana sahihi za maneno na tamathali za usemi tulizotumia kufanya ulinganishi pamoja na miktadha ya maneno hayo.

### 1.9.2 Watoa Habari

Tuliteua watoa habari kwa kutumia kielelezo makusudi ambao walisaidia katika kujaza maswali kwenye hojaji. Watoa habari hao walikuwa wazungumzaji asilia wa lugha ya Ekegusii wake kwa waume, wenye umri zaidi ya miaka arobaini kwa chukulio kwamba hao wanaelewa zaidi lugha kimuktadha.

### 1.9.3 Hojaji

Katika utafiti huu, hojaji ilitumika kukusanya data. Hojaji hiyo ilikuwa na kauli ambazo maana zake zingeelezwa na watoa habari.

### 1.9.4 Uwasilishaji wa data na uchanganuzi wake

Data ambayo talikusanya iliwasilishwa na kuchanganuliwa kwa misingi ya Nadharia ya ya Uhusiano na kanuni zake. Data hiyo ilisaidia kupima uhalali wa nadharia tete na madhumuni ya utafiti huu.

# SURA YA PILI

# KATEGORIA ZA KISEMANTIKI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inajadili kuhusu kategoria za kisemantiki. Kategoria hizo huainishwa kutegemea uamilifu wazo katika lugha. Katika kufanikisha upitishaji wa ujumbe, uteuzi mwafaka wa mbinu itakayotumiwa na msemaji hufanywa kwa chukulizi kwamba msikilizaji atatumia uwezo alio nao kufikia maana iliyokusudiwa na msemaji, katika muktadha fulani. Maarifa waliyo nayo wanajamii huwawezesha kusimba na kusimbua maana katika mazungumzo na hivyo kufanikisha mawasiliano. Usemaji ni suala la kihisia na maingiliano ya kimaarifa hufanywa kwa kutumia lugha. Ufasiri sahihi unapofikiwa, washiriki wa mazungumzo huwa wamefikia uhusiano (Sperber na Wilson, 2004).

Kategoria za kisemantiki ni mbinu inayotumiwa na jamii kuyapa maneno katika lugha zao maana. Kategoria za kisemantiki ni zile sehemu za lugha zinazosisitizwa katika utamaduni mahususi. Uainishaji wa maneno hutegemea miktadha ya matumizi ya maneno hayo katika utamaduni, hususan katika mawasiliano ya kimazungumzo ambapo lugha hudhihirika kiutendaji. Maneno fulani yanapotumika nje ya miktadha fulani huwa hayana maana maalum na hivyo ni lazima yafungamanishwe na maneno mengine kwenye tungo ili kuyapa maana (Ottenheimer, 2006).

Tamaduni nyingi huzingatia sifa za ubunifu na maingiliano ya watu, na utoaji wa maana ndio kusudi lao kuu, mara nyingi kwa kutumia chukulizi zisizosemwa

zinazosisitiza uteuzi na utendakazi wa kimakusudi. Watu wanaposhiriki mazungumzo huwa wanateua maneno kutoka kwa safu ya chaguzi ambayo yanafaa katika mazungumzo yao, katika miktadha ya wakati huo, na mara nyingi huwa wanazingatia kanuni za lugha kwa kutumia mbinu za ukiushi. Hali hii ya kukiuka lugha kimakusudi ndiyo hufasiriwa kama maana ya kimuktadha, ambayo hutumikiza kategoria za kimuktadha, na wala sio maana kileksika. ( Blommaert, 2005).

Rosch (1975) anatoa fafanuzi ya kategoria za kisemantiki kwa kuzigawa kwa makundi mawili makuu. Kategoria hizi zinaweza kubainika katika lugha zote. Kategoria zenyewe ni zile za kileksika pamoja na zile za kimuktadha.Kategoria hizi huelezwa kinadharia tu na wala sio kiutendaji kwa sababu hakuna mipaka inayobainika kati yazo.

**2.2 Kategoria za Kileksika**

Kategoria ya kileksika ndilo kundi la kwanza la kisemantiki ambapo vitu vyote vilivyo katika ulimwengu, vinavyoonekana na visivyoonekana hupewa majina ya kidhahania kimakundi. Makundi hayo si ya ubia bali hutegemea jamii-lugha, utamaduni wao na mazingira yao. Uainishaji wa vitu kimakundi hutokea bila kufahamu, kufikiri au kupanga. Hali ya ufahamu hutokea panapozuka utata. Rosch (1975) anaziita kategoria hizi za kisemantiki kategoria tambuzi. Kategoria hizi hupangwa na watumiaji wa lugha kutegemea tajiriba zao, imani na mazoea ya

jamii au kundi fulani la kijamii, na jinsi wanavyouona ulimwengu wao bila shaka itadhihirika kutokana na kategoria tofauti tofauti za kisemantiki. Kila kategoria huwa na kielelezo chenye sifa mahususi, na chochote kinachokiuka sifa za kundi hubainika kimaelezo na kuwekwa katika kundi lingine. Kwa mfano, kasuku anaweza kutumika kama kielelezo cha ndege ilhali popo ambaye ana sifa za ndege vilevile hutofautishwa na ndege kwa vile baadhi ya sifa zake ni tofauti na zile za ndege wengine.

Mbinu nyingine ya uainishaji ni ile iliyotumiwa na Voegelin (2006) na inazigawa kategoria za kisemantiki kwa matapo manne. Matapo hayo ni pamoja na 1) sura ya nchi pamoja na vitu na viumbe vilivyomo, 2) tabia na shughuli za watu, 3) shughuli za kiakili pamoja na hisia, jazba na maadili na, 4) watu na mahusiano kati yao. Katika kujumlisha matapo haya ya kusemantiki, Voegelin (Aprili 2006) katika makala ya AIATSIS anayaita makundi ya kisemantiki ambayo ni pamoja na nomino, vivumishi, vitenzi, na mengineyo anuwai yanayotoa maana msingi za dhana mbalimbali. Kategoria za kisemantiki zimerejelewa kama kategoria za kisintaksia na na kisemantiki na Bennet (2000).

Mbinu nyingine inayotumiwa kuainisha kategoria za kileksika ni ile inayoyagawa maneno ya lugha kwa makundi mawili makuu. Makundi hayo ni maneno makuu na maneno ya kimatumizi. Kundi la kwanza lina maneno mengi mno, na kila neno huwa na sura mbalimbali kutegemea jinsi linavyobainika kiuamilifu katika tungo.

Sura hizo zinatokana na uambishaji wa maneno hayo. Kundi la pili lina maneno machache, na maneno hayo huwa hayabadilikibadiliki (Crystal, 2003).

Maneno katika lugha hugawanywa katika sehemu mbalimbali kutegemea matumizi yayo katika upatanisho wa kisarufi. Migao hiyo ndiyo huitwa aina za maneno. Kila lugha ina maneno mengi yanayotumika katika mawasiliano ya kawaida na yale yanayotumika katika miktadha na taaluma maalum, na uianishaji huo hutegemea maana au semantiki, maumbo ya maneno hayo au mofolojia yao pamoja na uamilifu wa maneno hayo kwenye tungo, (Kapinga, 1983 ; Mgullu, 1999).

Nyanja za kileksika ndizo huorodheshwa kwenye makamusi ya lugha na maana za kila neno kuelezewa. Pamoja na maana msingi ya neno, matumizi yake pia huelezwa pamoja na jinsi neno hilo hubainika kimatumizi. Kando na matumizi yake, maneno huelezwa kama ni ya umoja au wingi, miktadha yanamotumika pamoja na makundi yao. Katika ufundishaji wa sarufi, maana msingi za maneno husisitizwa pamoja na taratibu za upanganji wa maneno hayo kenye tungo ili maana ziweze kufasiriwa kwa urahisi.

Kategoria za kileskika zimeelezwa kama aina za maneno katika lugha za Kiswahili na Ekegusii (Whiteley, 1956 ; Massamba na wenzake, 1999 ; Habwe na Karanja 2004). Katika lugha ya Kiswahili maneno yameainishwa kwa makundi manane

makuu ambayo ni nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi, vielezi, viunganishi, vihusishi na vihisishi. Majina ya makundi hayo yanatokana na uamilifu wayo katika sintaksia. Katika lugha ya Ekegusii makundi yaliyotambuliwa na Whiteley (1956) ni pamoja na nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi, vielezi, viunganishi, vihusishi na vihisishi. Taratibu hizi za uainishaji wa maneno katika lugha hizi mbili unaelekea kushabihiana kwa sababu lugha hizi zote ni za Kibantu na muundo wake wa kisintaksia unashabihiana sana.

Utafiti huu utachunguza kategoria mbili za kileksika ambazo hi nomino na vitenzi. Nomino ni maneno yanayotajia vitu, watu, hali na mahali. Kuna aina mbalimbali za nomino, (Mgullu, 1999 ; Habwe na Karanja 2004). Katika lugha za Kiswahili na Ekegusii, nomino zina mshabaha mkubwa kimaana na kiothografia, hasa ikizingatiwa kuwa hizi zote ni lugha za Kibantu. Mifano ya nomino ni :

| Kiswahili | Ekegusii |
|---|---|
| Mtu | *Omonto* |
| Nyumba | *enyomba* |
| Utamu | *obwansu* |
| Kuku | *engoko* |
| Maji | *amache* |
| Munyu | *omonyo* |

Maneno haya yana maana mahususi zinazoeleweka yanapoelezwa bila miktadha ya kimazungumzo. Tofauti na maana msingi za maneno haya, neno linapowekwa kwenye muktadha kimazungumzo linapata maana nyingine, kwa mfano:

3. *Mainye n'achete enyomba yaye.*

   Mainye anaipenda nyumba yake.

Kando na maana msingi ya nyumba, nomino hiyo inapata maana nyingine ambayo inadhihirika kiusemi kwamba:

Mainye anaipenda familia yake

Mazungumzo yanaliwezesha neno 'nyumba' kusimba maana nyingine tofauti na uwazi na hivyo kuzua umaanisho wa familia.

Vitenzi ni maneno yanayoeleza mambo yanayotendeka. Massamba (2004) anaeleza kitenzi kama 'Kipashio kinachotoa taarifa kuhusu tendo linalofanyika, lililofanyika au litakalofanyika.' Lugha zote zina maneno ya kutajia vitendo. Lugha za Kiswahili na Ekegusii zina vitenzi vingi ambavyo hubainisha mlingano wa kimuundo. Mifano ya vitenzi katika lugha hizi ni:

| Kiswahili | Ekegusii |
| --- | --- |
| Amka | *booka* |
| Funga | *sieka* |
| Toka | *sooka* |
| Angalia | *rigereria* |
| Lala | *raara* |

Maana msingi za vitenzi hivi katika lugha hizi ni mahususi. Hata hivyo, kimazungumzo vitenzi hivi huweza kupata maana nyingine tofauti na maana za kileksika, na maana hizo zinaweza kufikiwa na msikilizaji kwa kutumia mbinu ya ufaafu katika miktadha maalum, kwa mfano, mtu akisema;

4. *Tom nere <u>osieka</u>*

   Tom ndiye <u>alifunga</u>

Uwazi wa kauli hii ni kwamba Tom ndiye alifunga (pengine mlango) lakini umaanisho wake katika mazungumzo ukawa unaelekea kwenye ile hali ya kuwa wa mwisho katika mashindano fulani. Washiriki wa mazungumzo haya ni lazima wawe katika hali sawa ya kimawazo ili kupata maana ya kile kilichomaanishwa ingawa hakikusemwa kwa kutumia mbinu za uhusiano.

## 2.3 Kategoria za Kimuktadha

Kategoria za kimuktadha hushughulikia mahusiano ya kisintaksia kati ya kipengele kimoja kwenye sentensi pamoja na vipengele vingine ambavyo vinapotumika katika muktadha mmoja huwa na maana tofauti na ile maana ya kileksika iliyozoeleka ama inayofahamika. Kategoria hii ya kisemantiki aliyorejelea (Rosch 1975) kama kategoria ya kimuktadha aliifananisha na kiunzi cha utambuzi yenye fasiri tofauti na fiche katika muktadha mahususi. Kwa mfano, katika lugha ya Ekegusii, mtu akisema:

5. *Koranche ninchwo <u>onache</u>*

   Tafadhali njoo <u>unikate</u>

Hii ni tafsiri ya juujuu ambayo siyo maana iliyokusudiwa na msemaji. Katika muktadha wa kazi shambani watu wanapokuwa wakilima, mpokezi wa tamko hili ataelewa kwamba msemaji anamwambia yule msikilizaji aende amsaidie kukamilisha sehemu yake na wala si kwamba anataka msikilizaji amkate kwa kifaa chenye makali kama inavyoeleweka kauli hiyo kileksika. Msemaji wa kauli hiyo anamwelekeza msikilizaji wake kwenye muktadha ambapo kile kinachokatwa si yeye bali ni sehemu ya kazi inayofanywa. Ufahamu wa ufaafu pamoja na uwezo wa msikilizaji kusimbua maana zilizosimbwa na maneno kwenye kauli kutamsaidia kupata maana ya msemaji.

Maneno katika lugha hupata maana mpya yanapotumika kimuktadha. Katika tamko:

6. *Moraa <u>osookire</u>*

   Moraa <u>ametoka,</u>

kauli hii inaweza kupewa fasiri ya kileksika kama ilivyotolewa hapo juu iwapo ni tamko lililotolewa bila kuzingatia muktadha maalum. Hata hivyo, kutegemea muktadha pamoja na wahusika wa mazungumzo, kauli hii inaweza kuwa ilikusudiwa kuzua umaanisho ufuatao.

a) Moraa ameenda nje ya nyumba


b) Moraa ameolewa

c) Moraa ameenda msalani

d) Moraa aliwahi kufanya usherati.

Maana zinazozuka zina utata unaoweza kuelezwa kama umaanisho kwa vile kategoria za kisemantiki na za kimuktadha huwa hazitegemei maana za kileksika, (Thomas, 1995), kuwa miktadha inapobadilika, maana za maneno pia hubadilika.

Maana hizo zinaweza kufafanuliwa na mchoro wa Grice uliopambanuliwa na Levinson (2000) kwa njia ifuatayo:




Mabadiliko ya maana ya kisemantiki hutokana na fahamu za kitamaduni pamoja na Kanuni ya Upole ambayo huwaelekeza wazungumzaji kuepuka matumizi ya maneno yanayoweza kuwa na hisia na athari hasi kiusemi, (Leech, 1983, Thomas, 1995). Maana ya neno inahamishwa na kupewa maana nyingine neno fulani linapotumika katika mazungumzo kutokana na ukweli kwamba lugha sio kitu kilichosimama. Maana za kileksika zinaweza kupanuka na neno likabeba maana nyingine na hivyo kutumika kama kisawe cha neno lingine katika muktadha wa

mazungumzo, (Ullman, 1970,Macdonell, 1986). Neno linaweza kuzua utata iwapo lina maana zaidi ya moja likitumika katika muktadha usio wazi.

## 2.4 Uainishaji wa Kategoria za Kimuktadha

Kategoria za kisemantiki zinazotumika kimuktadha zinarejelewa kama mbinu za lugha na tamadhali za usemi. Kategoria za kisemantiki zinaweza kubainika kama neno moja, kishazi au sentensi nzima ambazo fasiri yake hutofautiana na maana yake ya kimsingi. Wakati mwingine mbinu za lugha pamoja na tamadhali za usemi zinaweza kuwa aina fulani ya marudio, mpangilio maalum au kuacha maneno fulani yenye maana mahususi au kifungu chenye maana maalum kama vile huwa inabainika kwenye nahau, istiari na uhuishi. Tamathali za lugha ni nyingi mno kutegemea lugha na utamaduni wa jamii mbalimbali. Katika mazungumzo, tamathali ambazo hutumika sana ni pamoja na tashibihi, istiari, taashira, tashihisi, chuku pamoja na vijembe miongoni mwa nyingine. (Kuhenga, 1977, Wamitila 2001). Mbinu za lugha ni methali na nahau. Kwa sababu ya upana wa kila mojawapo ya mbinu hizi pamoja tamathali hizi, utafiti huu utajikita kwenye uchanganuzi wa methali na nahau kama mbinu za lugha. Vilevile tulichunguza sitiari tashbihi na taashira kama zinavyobainika kimazungumzo miongoni mwa jamii za Abagusii na Waswahili na uwazi na umaanisho zinazozua.

### 2.4.1 Mbinu za Lugha na Tamathali za Semi

Maelezo mengi yanayotoa maana ya methali yanakubaliana kwamba methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yaliyotumiwa, (TUKI, 2004). Wamitila (2001) katika utangulizi wake anaeleza methali kama "msemo unaojitosheleza, wenye maana yenye nguvu au uzito, wenye muundo au sifa ya kishairi unaokusudiwa kuadibu, kuelekeza, kuelimisha, kushauri na kadhalika". Arege na Nyanje (2011) wamezieleza methali kama "tungo fupi ambazo zina maana pana, na ambazo zinaeleza kwa ufupi mawazo, tajiriba, mafunzo pamoja na falsafa ya jamii". Methali hupamba au kukamilisha wazo katika tanzu nyingine za fasihi kama vile hadithi au mazungumzo.

### 2.4.2 Methali

Katika mazungumzo ya kijamii, methali hutumiwa na wazungumzaji kwa nia ya kuipamba lugha, kufupisha maelezo, kuelimisha pamoja na kufahamisha. Methali hazitumiki tu kiholela ila mzungumzaji huteua methali itakayoafikia lengo la ujumbe alio nao na kuzua umaanisho utakaofasiriwa na msikilizaji wake kwa njia aliyokusudia yeye msemaji. Hali hii hufanikisha mazungumzo kwa vile methali husimba maana zinazohitaji kufasirwa kiuwazi na kiumaanisho ili kufikia makusudi ya mawasiliano. Kwa mfano, baada ya mtu mzee kumshauri mtoto wake atamwambia:

7. *Yaa inyora* <u>*monto monene n'riogo*</u>

Kijana kumbuka <u>mtu mzima ni dawa</u>,

Hii ni fasiri ya kileksika na siyo iliyokusudiwa. Katika jamii ya Waswahili angetumia methali, kumbuka,

Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Jamii inachukulia kuwa ushauri unaotolewa na mtu mzima au mtu mzee kwa kijana utamfaa sana na kumwepusha na madhara, kama vile dawa hutibu ugonjwa. Hivyo maneno ya methali hii yanasimba maana kwamba ushauri wa mtu mzima ni sawa na dawa inayotibu upumbavu unaoambatana na ujana.

### 2.4.3 Nahau

Nahau ni misemo ya picha ambayo huwa na maana iliyofichika. Nahau huwa na undani wa kimaana kuliko baadhi ya misemo inayopatikana katika lugha nyingine. Kimuundo, nahau huwa na kitenzi na jina (Wamitila, 2003, TUKI, 2004) wanaeleza nahau kama fungu la maneno lenye maana maalumu isiyotokana na maana za kawaida za maneno yaliyotumiwa.

Lugha zote zina utajiri mkubwa wa nahau kutegemea tamaduni na mazingira yao. Nahau hutumika katika miktadha rasmi na hata kwenye lugha za misimu. Vilevile, nahau hutumika kwenye mashairi pamoja na tungo nyingine za kifasihi na hata katika Biblia. Naye Stamenkovic (2010) katika utangulizi wa toleo la jarida la *Meaning Shift* anasema kuwa nahau hazizingatii utaratibu wa lugha uliozoeleka

kikaida na hivyo basi maana inayozuka kutokana nazo ni tofauti na fasiri ya uwazi. Katika kufasiri nahau watumiaji wa lugha hurejelea hisia, matendo na athari zinazohusiana na sehemu mbalimbali za mwili wa binadamu na vitu vingine vilivyo katika mazingira yao. Sehemu za mwili ni kama vile kichwa, mkono, moyo, kidole, jino, sikio na kadhalika, hali ambayo hufanya urejelezi kueleweka kwa urahisi katika jamii zinamotumika nahau husika. Hoja hiyo inaungwa mkono na Farsi (1973, Kuhenga, 1977).

Nahau hutenda kazi kama neno moja kwa vile maana inayozuka huwa dhana moja pekee. Kwa sababu hiyo, tungo zinazochukuliwa kama nahau katika lugha haziwezi kuvunjwavunjwa, na kutengwa kwa vijenzi vyake kutasababisha kupotea kwa maana. Ni nadra sana kupata nahau katika lugha na tamaduni mbili tofauti zinazoshabihiana kimuundo na kimaana. Uelewa wa nahau za lugha moja hauwezi kumwelekeza mtu kuzielewa nahau katika lugha nyingine kwa sababu nahau hutegemea miktadha na tamaduni ambazo hutofautiana kutoka kwa jamii moja hadi nyingine. Kwa mfano, katika lugha ya Ekegusii, kauli :

8. *Gosooka kabere,*

   Kutoka mara mbili

Kauli hii ina maana kwamba mtu anayerejelewa huwa anatoka mara mbili. Hii ni maana ya uwazi ya kauli hii ambayo inaumaanisho kuwa yeye ni mchawi kwa sababu katika jamii hii mchawi hutoka nje mlango ukishafungwa wakati watu wamelala na kwenda kuroga. Jamii ya Waswahili wakimrejelea mtu mwenye tabia

kama hiyo watasema moja kwa moja kuwa fulani ni mchawi au mshirikina. Aidha, huku kutoka mara mbili kunaweza kufasiriwa kumaanisha hali ya mtu kwenda msalani mara kadhaa kutokana kutibukwa na tumbo linaloendesha. Uteuzi huu wa maneno unaelekezwa na kanuni ya upole ili kuziba pengo kati ya watu wa umri au jinsia tofauti.

Nahau huambatanishwa na maneno mengine kwenye tungo ili kuzipa uzito na mwelekeo wa kitu, mtu an hali inayorejelewa. Hii ndiyo maana huwa zinabainika wazi zaidi  kimatumizi katika mazungumzo ya kijamii ambapo mara nyingi mambo yanayozungumziwa ni porojo au umbeya kuhusu watu ambao wako katika miktadha husika lakini wanachukuliwa kuwa hawako, watu wa jamii-lugha nyingine, watoto wadogo, watu wazee sana au wagonjwa ambao katika mazungumzo wahusika wanachukulia kuwa hawaelewi kile kinachosemwa; (Wadensjo 1998). Nahau hutokea kama kiungo muhimu sana katika mazungumzo kwa kusimba maana zenye umaanisho.

### 2.4.4 Tashibihi

Tashibihi hutokana na neno la Kiswahili ‘shabihi’ lenye maana ya kufanana, kulingana au kuwa sawasawa na. Vitu viwili hulinganishwa kwa njia ya wazi wazi kwa kutumia viungo kama vile ‘mfano wa’, ‘kama’, mithili ya’, ‘ja’ na kadhalika. (Kuhenga, 1977, Wamitila, 2003). Tashbihi hutumika kusisitiza kauli na kuepuka maelezo mengi. Tazama mfano huu katika lugha ya Ekegusii.

9. *Ng'ai mokorwo monga* *__buna ching'uko__*?

Mnatoka wapi mnakaa __kama fuko__?

Kauli hiyo inapotolewa na mama akiwagomeza watoto wake anawafananisha na fuko, ambao katika muktadha husika ni kigezo cha uchafu; yaani wamejaa vumbi kila mahali, jinsi mwili wa fuko huonekana. Lengo kuu la kutumia tashbihi ni kusisistiza.

Ijapokuwa watoto hao hawamuoni fuko, ufahamu kwamba anaishi ardhini unawaelekeza kuihusisha hali yao na fuko na hivyo wakatambua kuwa wamechafuka mno. Fuko anatumiwa kuwakilisha uchafu, na msemaji anazua umaanisho kwa kutumia badala ya maelezo ya moja kwa moja ambayo huenda yasitoe msisitizo sawa na huo.

### 2.4.5 Taashira

Taashira ni tendo, kitu au mtu atoaye ishara, dokezo au alama kufidisha kitu kingine (Kuhenga 1977, Wamitila, 2003). Badala ya kutumia maneno mengi au maelezo marefu kumwambia mtu jambo, wazungumzaji hutumia taashira kuafikia maana kwa njia ya moja kwa moja, ingawa maana yenyewe huhitaji juhudi ya msikilizaji ili kuifikia. Kwa mfano, katika mazungumzo mtu anaweza kusema;

10. *Nigo okoganya* *__goika chimbuche chimere omotwe__*

Utangoja __hadi mvi ziote kichwani__

Yule anayeelekezewa kauli hii anaonywa dhidi ya kungoja kwa sababu huenda kile au yule anayemngoja asiwahi kuja au kutimiza alichotarajiwa kutimiza. Mfano mwingine ni:

11. *Irana inka <u>obwate ekebago</u>*

Rudi nyumbani <u>ushike mpini</u> au

Rudi nyumbani <u>ukamate jembe</u>

Kauli hiyo pia inarejelea ukulima kwa matumizi ya mpini au jembe. Mvi na jembe ndizo taashira kwenye kauli hizo.

Taashira hizo zinasimba ukulima na uzee kwa vile ni vitu vinavyoeleweka katika fahamu za watumizi lugha na pia kuonyesha takrima, (Leech, 1983). Uwezo wa msikilijazaji kupata maana ndio unafanikisha uhusiano na ufaafu wa ujumbe. Uelewa unapofikiwa ndio unaifanya kauli hiyo kuwa na ufaafu kwa msikilizaji, ingawa ujumbe wenyewe haujasemwa na mtoaji wa kauli.

### 2.4.6 Sitiari

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo kwayo kitu, matendo au vitu vyenye hulka na sura mbalimbali hulinganishwa na hali sawasawa na maumbile au jinsi ya utendaji. Maneno ‘kama’, ‘kwa mfano’ na ‘kama vile’ hayatumiki. Sitiari ni dhana inayotokana na neno ‘sitiri’, lenye maana ya kuficha au kufunika. (Kuhenga, 1977, Wamitila, 2003) Sitiari kama dhana inayoeleza sifa ya kitu fulani kwa kusema kuwa ni kingine. Maana huwa inahamishwa kwa vile hakuna matumizi ya viungo. Kwa mfano:

12. *Momanyi <u>n’engabi</u>*

Momanyi <u>ni swara</u>

Kauli hii ina maana kuwa Momanyi ana mbio sana. Ulinganishi huu wa kiubunifu huweka msisitizo katika kile kinachosemwa. Katika kuelewa kauli hii, msemaji

anayabana maneno mengi na badala yake anatumia neno moja ambalo msikilizaji wake atalipanua kwa kutumia ufaafu kuifikia maana iliyokusudiwa, kwamba Momanyi ana mbio sana kwa kumfananisha na swara.

Hizi ni baadhi tu za tamadhali za semi katika lugha ambazo hubainika kimazungumzo, japo mazungumzo yatakuwa rasmi au yasiyo rasmi katika jamii na lugha zote. Tamadhali hizi zimeelezwa na wanapragmatiki kama kategoria za kimuktadha kwa vile maana yazo hubainika wazi katika miktadha maalum. Aidha, maana za kategoria hizo ni fiche na hivyo huwa zinazuia umaanisho zinapotumika.

## 2.5 Hitimisho

Katika sura hii, kategoria za kisemantiki zimejadiliwa. Kategoria za kisemantiki ni pamoja na zile za kileksika na kateoria za kimuktdha. Kategoria za kileksika zimeelezwa kama kategoria tambuzi ambazo hueleza maana msingi ya maneno katika lugha, na ndizo wanaisimu wameeleza kwenye makamusi ya lugha. Kategoria za kileksika pia zimeainishwa kama kategoria za maneno ambayo uainishaji wake hutegemea miundo yake kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Nazo kategoria za kimuktadha zimeelezwa kama tamadhali za lugha ambazo huwa ni neno, kishazi au sentensi nzima ambayo huwa na maana tofauti na ile maana ya kileksika hasa zinapotumika katika miktadha mbalimbali kimazungumzo. Kimatumizi, kategoria hizi huingiliana hivi kwamba ni vigumu kuweka mipaka kati ya kategoria za kileksika na kategoria za kimuktadha kimatumizi katika lugha ya mazungumzo.

# SURA YA TATU

# KATEGORIA ZA KISEMANTIKI ZA KISWAHILI NA EKEGUSII

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, kategoria za kisemantiki ambazo ni aina za maneno pamoja na tamathali za semi katika lugha za Ekegusii na za Kiswahili zitajadiliwa. Maneno ndiyo hutumiwa katika mazungumzo. Kategoria za kisemantiki katika lugha zote huwa na makundi mawili makuu ya maneno. Maneno hayo huitwa maneno makuu ambayo ni pamoja na nomino, vivumishi, vitenzi na vielezi. Maneno haya ni mengi mno katika lugha zote yakilinganishwa na yale ya kundi la pili. Miundo ya maneno haya hubadilikabadilika. Kundi la pili la maneno ni lile la maneno ya kimatumizi ambayo ni machache na huwa hayabadilibadiliki kimuundo. Kwa sababu ya kutobadilika huko, idadi ya maneno hayo si kubwa. Katika kundi hili kuna viunganishi, viwakilishi, vihusishi na vihisishi (Crystal, 2003). Kategoria za kileksika ambazo tutazichanganua ni zile za nomino na vitenzi pekee ilhali kategoria za kimuktadha tutakazochua ni methali, nahau, tashibihi, taashira na istiari.

Kategoria za kisemantiki zimeelezwa kama mbinu inayotumiwa na jamiilugha kuainisha maneno katika lugha zao (Mgullu, 1999; Habwe na Karanja 2004). Hata hivyo, katika uchunguzi huu tulizingatia zaidi aina za maneno ambayo yanapotumika kimazungumzo huwa yanazua utata na hiyo kufasiriwa

kiumaanisho, kinyume na maana msingi za maneno hayo kama yanavyoeleweka kikamusi. Kwa kuwa muktadha ni suala muhimu sana katika mazungumzo, ni muhimu kutaja kwamba kauli tutakazozichanganua ni zile zinazoibuka katika mazungumzo ya jamii, na jamii hapa inamaanisha mkusanyiko wa watu walio jumuika pamoja, wanaozungumza lugha moja na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kila siku kuwa na mitagusano ya mara kwa mara ya kimazungumzo.

Neno moja linaweza kuibua maana kadhaa katika mazungumzo au likamaanisha dhana tofauti katika miktadha miwili tofauti, mmoja ukiegemea hali ya ukanushi au ukiushi. Aidha, matabaka mawili tofauti ya watu yanaweza kutumia maneno yale yale na kuzua maana tofauti kutegemea yanatumika wapi na ni kwa malengo gani  (Macdonell, 1986).

Lugha za Kibantu zikiwemo lugha za Kiswahili na Ekegusii zina kategoria  nane kuu za kisemantiki (Guthrie, 1970, Kapinga, 1983, Mbaabu, 1985). Waandishi hao wanazirejelea kama sehemu za usemi ilhali Habwe na Karanja (2004) wanaziita viambajengo vya sentensi. Kategoria hizi zimeainishwa kimakundi kulingana na maana zake, miundo yake pamoja na uamilifu wazo katika sintaksia. Utaratibu unaokubalika zaidi wa muundo wa sentensi za Kibantu ni ule wa kirai nomino na kirai kitenzi  (Guthrie, 1970,  Massamba ,1999).

Tamathali za semi ni mafungu ya maneno au hata neno moja ambalo limegeuzwa maana yake ya kiasilia na kuwa na maana nyingine hasa kimatumizi kwenye mazungumzo, (Wamitila, 2003). Kando na jumbe zinazobebwa na tamathali za usemi, zinaonyesha uwezo wa kisanii alio nao mtumizi wake katika lugha na utamaduni wa jamii yake. Tamathali za usemi zinaundwa kutokana na kategoria za kisemantiki yaani ni tungo za kawaida ambazo zimekwezwa kimaana ili zitumike kuzua maana mahususi tofauti na maana za kileksika za maneno yanayoziunda. Muundo wa kimtindo unaotokana na tamathali za usemi ni ruwaza ya kimtindo unayotokana na uwezo wa msemaji ambao huhusishwa na lengo la msemaji. Kutokana na ukweli huu, mipaka kati ya kategoria za kimuktadha au tamathali za usemi na kategoria za kisemantiki ni telezi mno na maelezo tutakayozingatia ni yale yanayohusiana na miktadha ya kimazungumzo pekee katika jamii.

### 3.2 Kategoria za Kisemantiki za Kiswahili

Lugha ya Kiswahili kama lugha nyingine za Kibantu ina kategoria nane za maneno ambayo hutajia dhana na vitu mbalimbali. Kategoria hizi ni pamoja na nomino, viwakilishi, vivumishi, vitenzi, vielezi, viunganishi, vihusisi na vihisishi. (Kapinga, 1983) anasema kuwa makundi hayo ya majina kwa kadiri ya upatanisho wa kisarufi ulio baina yao na vivumishi, viwakilishi, au vitenzi huitwa ngeli. Kuna ngeli kumi na tano za majina katika lugha za Kibantu ambazo zimeainishwa kwa njia tofautitofauti kutegemea muundo, maana na uamilifu wake.

### 3.2.1 Nomino za Kiswahili

Kulingana na Mgullu (1999), ‘Nomino ni maneno ambayo hutaja vitu. Kwa hivyo nomino hutaja majina ya watu, vitu, mahali, vyeo, dhana na hata tendo. Ndiyo maana wanaisimu wengine wanaziita nomino majina’ uk 136. Kutokana na maelezo haya, nomino ni neno linalotaja kitu fulani kukitofautisha au kukipambanua miongoni mwa vitu.majina ya watu, vitu na mahali yamegawanywa kimakundi kwa kuzingatia uwiano wa majina hayo pamoja na vitenzi vinavyoaarifu. Kapinga (1983) anasema kuwa makundi hayo ya majina kwa kadiri ya upatanisho wa kisarufi ulio baina yao na vivumishi, viwakilishi, au vitenzi huitwa ngeli. Kuna ngeli kumi na tano za majina katika lugha ya Kiswahili ambazo zimeainishwa kwa njia tofautitofauti kutegemea muundo, maana na uamilifu wake.

Katika semantiki, nomino kama neno huru linalotajia vitu, watu na mahali, huwa na maana mahususi kwa kuwa huwa linaeleza maana msingi ya nomino inayotajwa. Habwe & Karanja (2004) wanasema kwamba :

> ‘Maana katika kiwango cha neno huru huitwa maana kileksika. Hii hurejelea maana ya msamiati wa lugha. Maana hii huwa ni ile inayowakilishwa na vidahizo katika kamusi…. Maana msingi ndiyo maana kuu ya neno…. Maana hii huwa haibadiliki kutegemea athari za kimazingira au kimuktadha’ uk 205.

Fahiwa nyingine zitakazoibuka zinahusiana na maana msingi ya neno. Hiyo basi, hata katika mazungumzo au aina nyingine ya mawasiliano, mtoaji wa kauli hulenga kupitisha ujumbe kwa kutumia nomino fulani, na ujumbe huo hutokana na maana itakayoibuka, na ambao ndicho kipengele muhimu zaidi katika mawasiliano. Hata hivyo, katika harakati za kupitisha ujumbe, nomino zinazotumiwa zinazua utata ambao msikilizaji anahitajika kuusimbua ili kuufikia ujumbe uliosimbwa kwenye kauli ya msemaji. Kwa kukiuka baadhi ya kanuni za Grice (1975). Kauli zifuatazo zinaweza kubainisha hali hiyo :

13. Juma anajenga <u>ghorofa.</u>

14. Mchezaji alionyeshwa <u>kadi nyekundu.</u>

15. Ken atanunua <u>benz.</u>

16. Hamisi alioa <u>mwanamke</u>.

Nomino zilizopigiwa mistari ni maneno ya kawaida. Hata hivyo, kimatumizi kwenye kauli za kimazungumzo, msikilizaji anatambua kwamba kuna jumbe nyingine zaidi ya maana za kileksika za nomino hizo, ambapo msikilizaji anaweza kufasiri kuwa

ghorofa – jumba la kifahari

kadi nyekundu – ni kupigwa marufuku kushiriki kwenye mashindano

Benz – gari la fahari au utajiri

Mwanamke – mke mwenye sifa nzuri.

Mpokezi wa kauli hizi anazingatia mkondo wa ufahamu unaotumikiza juhudi kidogo zaidi iwezekanavyo ili kuufikia ujumbe kwenye kauli hizo pamoja kwa

kuzitathmini nadharia tete zilizoko kwenye kauli hizo pamoja na utata, urejelezi na umaanisho wake. Iwapo utaafikia fasihi sahihi basi atakuwa ameafikia umaanisho (Sperber & Wilson, 1986 ; Yule 1996) anasema kwamba ili mpokezi wa kauli hizo aweze kuzifasiri kwa usahihi, ni lazima awe na mbinu na taratibu za kiufahamu za awali zitakazomwezesha kuzichanganua kauli hizo, na mbinu hizo hutokana na elimu na uwezo wa kuelewa utamaduni mnamotumika dhana hizo. Wazungumzaji hutumia nomino fulani kusimba maana ya dhana nyingine. Msemaji hutoa kauli yenye maana iliyo isiyo wazi ilhali msikilizaji anajukumika kutambua maana ya kile alichokusudia msemaji na kuisimbua maana kwa kutumia urejelezi, muktadha na ufaafu wa ujumbe ambao utamwezesha kupata maana iliyokusudiwa ingawa haikubainika kiusemi.

### 3.2.2 Vitenzi vya Kiswahili

Kitenzi ni aina ya neno linaloarifu aina ya nomino au tendo linalofanyika. Kitenzi huarifu linalofanywa na mtu, mnyama au kitu kingine chochote. Kitenzi kinaweza kuambishwa ili kulipa neno maana mahususi (Mgullu, 1999, Habwe & Karanja, 2004). Viambishi ambavyo huongezwa kwenye vitenzi husaidia kubainisha njeo, hali, idadi, dhamira, kauli na pia kuwakilisha kiima. Kutokana na jukumu la vitenzi katika mawasiliano, vinabainika kama kategoria muhimu sana ya kisemantiki kwa kuwa vinatoa ujumbe kuhusu nomino, kwa mfano :

17. Babu amelala.

18. Nitakuona kesho.

Katika matamko yenye vitenzi 'lala' na 'ona', watoaji wa kauli wametoa ujumbe unaoeleweka. Hata hivyo, wanachosema sicho wanachokimaanisha. Katika kauli hizi, umaanisho unaibuka kwa kuwa vitenzi hivyo vinazua maana zifuatazo :

Kulala – kufa

Ona – kuzungumza na mtu au kumlipa mtu deni lake

Kitenzi 'ona' huchukuliwa kuwa na maana ya kutazama kwa kutumia macho lakini katika muktadha huu kitenzi hicho kinaibua maana tatu, kwamba kwa upande mmoja kuna hali chanya ilhali mwathiriwa wa kitendo hicho anapata hisia hasi. Umaanisho unaafikiwa kwa kuhusisha matamko hayo na miktadha pamoja na jumbe za awali alizo nazo msikilizaji na hivyo kunazuka ukiushi wa maana msingi ya vitenzi vilivyotumika (Thomas, 1995). Mzungumzaji anamaanisha kwamba 'babu amekufa' katika kauli ya kwanza na katika kauli ya pili, fasiri zifuatazo zinaweza kuafikiwa ; kwamba atashauriana na mpokezi wa kauli kesho yake au iwapo ni kitu fulani alikuwa amletee basi atatimiza ahadi hiyo keshoye. Hapa, kitenzi 'ona' kinapata maana iliyopanuliwa kwa matilaba ya kuwasiliana na msikilizaji anateua umaanisho ambao utamsaidia kuelewa kusudi la msemaji.

Mfano mwingine wa kauli yenye kitenzi kinachozua utata ni.

19. Tulimtema Margy kutoka kwa chama chetu.

Kitenzi 'tema' kimsingi kina maana ya 'kutupa kutoka mdomoni ' au 'kukata sehemu ya kitu'. Kitenzi hiki kimetumika katika kauli hii kiumaanisho ambapo maana yake ya kimsingi imehamishwa na kuwekwa katika muktadha ambapo

kinazua umaanisho wa kufukuza. Jinsi inavyotokea katika hali halisi mtu anapokata sehemu ya kitu au kutupa kitu au mate kutoka mdomoni, mzungumzaji anakuwa na matarajio kwamba mpokezi atasimbua ujumbe uliosimbwa na kitenzi kutema na kupata fasiri kwamba mrejelewa amefukuzwa chamani.

### 3.3 Kategoria za Kisemantiki za Ekegusii

Lugha ya Ekegusii ina kategoria nane za kisemantiki ambazo zimeelezwa na Whiteley (1965). Muundo wa lugha hii ni sawa na ule wa lugha ya Kiswahili. Konsonanti na vokali za Ekegusii na Kiswahili zinafanana. Kimsingi, kategoria za maneno ya Ekegusii ni sawa na za Kiswahili. Tofauti zinazobainika ni zile za kimuundo ambapo lugha ya Ekegusii ina baadhi ya majina ya nomino tofauti na Kiswahili. Kategoria za kisemantiki za Ekegusii ni pamoja na nomino, vivumishi, viwakilishi, vitenzi, vielezi, vuinganishi, vihusishi na vihisishi. Kategoria hizi huelezea dhana mbalimbali katika lugha na ndizo zinazoeleweka kimsingi kubeba maana za dhana mbalimbali. Licha ya hali hii, wazungumzaji huhamisha maana za kategoria hizi na kuyatumia kana kwamba yana maana nyingine zaidi ya ile inayoeleweka kimsingi. Tutachanganua nomino na vitenzi katika lugha hii ili kubaini jinsi maneno hayo yanavyozua utata.

### 3.3.1 Nomino za Ekegusii

Lugha ya Ekegusii kama lugha nyingine za Kibantu ina ngeli kumi na tano za nomino. Nomino hizo zinataja majina ya watu, vitu, mahali, hali na matendo. Baadhi ya nomino za Ekegusii ni pamoja na :

| Ekegusii | Kiswahili |
|---|---|
| *Baaba* - | mama au nyanya |
| *Eriiso* - | jicho |
| *Amaanyinga* - | damu |
| *Omote* - | mti |

Wazungumzaji wanaweza kutumia nomino hizo kwa njia ya umaanisho na kuzua maana nyingine tofauti kabisa na maana msingi za maneno hayo, kwa mfano:

20. *Sam n'eriiso erimo* (Sam ni jicho moja)

Jicho ni sehemu inayotumika kuona. Fasiri ya uwazi ya kauli hii ni kuwa Sam ana jicho moja au yeye ni chongo. Maana ya umaanisho ya kauli hii ni kwamba Sam ni mtoto wa pekee wa wazazi wake na hivyo, wazazi wake ndio wanalinganishwa na mtu ambaye ni chongo. Katika tamaduni za Abagusii na imani zao pamoja na malengo ya kusisitiza, mtoto anayezaliwa peke yake hulinganishwa na jicho moja ambalo huhitaji uangalifu mkubwa kulitunza la sivyo mwenye jicho hilo apoteze uwezo wa kuona. Upofu unalinganishwa na kule kukosa mtu wa kuendeleza kizazi chake.

21. *Intwe n'amaayinga ayaamo* (sisi ni damu moja)

Msemaji anapotua kauli hii huwa analenga kupitisha ujumbe kwamba wana uhusiano wa kiukoo. Hali hii inarahisishwa na muktadha wa usemi pamoja na jumbe za awali na imani za wahusika zinazomuelekeza msikilizaji kupata umaanisho bila kutumia juhudi nyingi.

Nomino ‘omote’ mti ina maana mahususi. Nomino hii ikiwekwa kwa wingi ‘emete’ katika Ekegusii inakuwa na maana mbili ; mimea yenye mashiria magumu, na dawa za mitishamba. Mzungumzaji atasikika akisema hivi :

22. *Kae omwana oyio emete akire*

Mpe mtoto huyo miti anyamaze

Maana ya juu juu ya kauli hiyo ni tata. Fasiri ya uwazi ya kauli hii ni kwamba mtoto apewe miti. Kutegemea muktadha wa mazungumzo kauli hii ina maana kwamba mtoto anayezungumziwa achapwe viboko ili aache kulialia ovyo. Miti inasimba maana ya kichapo au viboko, na fahamu hiyo inatokana na ukweli kwamba kiboko huchunwa kutoka kwa mti. Umaanisho wa mazungumzo, unawezeshwa na fahamu za awali kuhusiana na ujumbe unaotolewa pamoja na ufaafu wa ujumbe huo kwa mpokezi. Mpokezi anatumia ufahamu wa utamaduni pamoja na muktadha ambapo maana ya miti inahamishwa na kupewa maana nyingine katika muktadha wa mazungumzo (Sperber na Wilson, 2004).

### 3.3.2 Vitenzi vya Ekegusii

Mbaabu (1985) anaeleza kwamba vitenzi ni maneno ambayo yanaonyesha kwamba jambo fulani linafanywa. Katika vitenzi, viambishi huongezwa ambavyo ndivyo vipashio vinavyobeba hali, njeo, idadi dhamira, kiima na kauli. Baadhi ya vitenzi vya Ekegusii ni kama vile :

| Ekegusii | Kiswahili |
|---|---|
| *Goaaka* | kupiga |
| *Kogesa* | kuvuna |
| *Gosooka* | kuondoka (nje) |
| *Gosieka* | kufunga (mlango) |

Maana msingi za vitenzi hivyo na ulinganishi wake wa Kiswahili ni wazi na wa moja kwa moja. Hata hivyo katika kauli, hali hubainika kuwa tofauti. Tazama mifano ifautayo ya kauli :

23. *Embori eyio nero yaakirwe ekeranya*. (Mbuzi huyo ndiye aliyepigwa kiboko).

Hii ni tafsiri ya moja kwa moja ambayo haifikii maana ya kindani ya kauli 'gooaka ekeranya' au kupiga kiboko. Fasiri ya kimaarifa inamwelekeza mpokezi au mshiriki wa mazungumzo haya kwenye maana mbili. Maana ya kwanza ni kwamba mbuzi anachapwa kiboko, na maana hii ndiyo uwazi. Maana ya pili ambayo ndiyo maana ya kauli hiyo kiumaanisho ni 'kukitenga kitu kwa ajili ya shughuli fulani maalum'. Panapozuka tamko kama hili, msikilizaji analazimika kutathmini kauli 'gooaka ekeranya', yaani kupiga kiboko na kurejelea maana

nyinginezo kwa kukisia anachonuia msemaji, hasa mazungumzo yanapolenga wazo la uteuzi wa kitu kimoja miongoni mwa vitu vingi. Chukulizi za maana za kileksika pekee za maneno hasa vitenzi husababisha utata ambao ndicho kiini hasa cha ubunifu katika kazi za kisanaa (Thomas, 1995). Uelewa wa kile kinachosemwa unaafikiwa na msikilizaji, kwa kufasiri mana umaanisho ya kitenzi kilichotumiwa ambacho ndicho husimba maana ya umaanisho.

24. *Tweng'use mbaka bwoye* (twende hadi kwake).

Fasiri ya uwazi ya kauli hii ni kwamba 'tujivute hadi kwake.' Katika mazungumzo, mtu mmoja atasikika akimhimiza mwingine kwa matumizi ya kitenzi 'ngusa' yaani vuta. Mtu anapuvuta kitu hutumia nguvu akiwa na kusudi la kupata kitu kingine. Mzungumzaji anabadilisha kitenzi 'twende' na badala yake anatumia 'tujivute' kwa dhamira ya msisitizo pamoja na ukweli kwamba kujivuta ni tendo linaloonyesha lazima iliyoko ya kwenda kwa mwenzao.

Katika lugha ya mazungumzo, kunabainika ishara, maneno au kauli zinazotokana na maneno mengine yenye maana tofauti. Mtazamo wa kimapokeo ni kuwa uhusiano wa maneno unaoibuka katika mazungumzo huwa na mkazo fulani, yaani usemi unatokea tu kimafumbo na kuchukuliwa kama hali ya kawaida tu ya lugha kimatumizi. Maneno yaliyomo yanapoeleweka na jinsi yaliyounganishwa, basi maana za kauli nzima zinaweza kukisiwa. Hii ndiyo kanuni ya utungo, na ndiyo chukulizi ya kazi nyingi za kisanaa, kwani sanaa huundwa kwa kule kutoeleweka kwa maneno yanayotumiwa na wazungumzaji kwa njia ya moja kwa moja,

(Szabo, 2006). Dhana ambazo zinafanana au kuhusiana pia zinaweza kutumikiza vitenzi vinavyofanana na vikaeleweka na watumizi wa lugha ingawa kimsingi vitenzi hivyo hukusishwa na muktadha mahususi, kwa mfano kitenzi.

25. *Mary tari guata*

Kitenzi *ata* kinaposimama peke yake kina maana ya kuvunja, kama vile mtu anavyovunja chungu au yai. Hata hivyo, kitenzi hicho hutumika kimazungumzo ambapo kauli kama hii ni kawaida kimazungumzo. Maarifa ya kiufasiri humuwezesha mpokezi kutambua amakusudio ya usemaji pamoja na vidokezi vilivyomo kwenye muktadha wa mazungumzo. Uwazi unaozuka ni kuwa Mary ni mwangalifu na hivyo hawezi kuvunja kitu. Hata hivyo, umaanisho wake, unaoelekezwa na fahamu za awali ni kuwa Mary ni mzembe sana kiasi kwamba hawezi kufanya kazi yoyote, hata kama ni kuvunja yai ijapo ni jepesi mno kuvunjika.

26. *Koiyora* – kuepua (hasa chakula kutoka jikoni)

Katika muktadha wa kazi hasa ya ujenzi wa nyumba ambapo udongo huchanyanywa na maji na kasha kukanyagwakanyagwa na watu ili baadaye utumike kukandika kuta za nyumba, udongo ule unapokuwa tayari hulinganishwa na chakula kilichoiva na hivyo mtu atasikika akimwambia mwenzake. Fasiri inamfikia mpokezi kwa kuhusisha fahamu za awali na muktadha ili kupata maana iliyokusudiwa (Sperber na Wilson, 2004).

27. *<u>Iyora</u> esike eyio* (epua udongo huo).

Katika muktadha wa upishi ni kawaida kutumia ‘koiyora’ yaani ‘kuepua’ lakini kuhusiana na udongo uliotayarishwa pasipo moto, dhana ya kuepua inalenga maana ya kule kuwa tayari kutumika kwa udongo ule, sawia na ule inavyokuwa chakula kinapoiva.

Mbinu hii ya kuufikia umaanisho inatokana na kile wanapragmatiki wanaita upunguzaji wa kileksika ambao huathirwa na mazungumzo kutegemea muktadha, hali, wakati na watumizi wake ili kufanikisha ufaafu. Maoni haya yanaungwa mkono na Barsalous katika Sperber na Wilson (2004). Mazungumzo yanayotumikiza mbinu hii ya upunguzaji wa kileksika unadhihirika pia katika mazungumzo ya misimu miongoni mwa watu hasa wanaporejelea jambo au kitu ambacho kimekuwa tayari au kimekamilika, ambapo mtu atasikika akisema:

28. Ule mpango umeiva.

29. Msichana yule ameiva.

Urejelezi huu unaelekea kulingana na kauli ya Ekegusii ‘kuepua’ kwa vile vitenzi vyote viwaashiria nomino ambazo ziko tayari kimatumizi. Matumizi ya lugha kwa namna hii huzua matatizo kuhusiana na zile kanuni za Grice hasa ya ukweli kwa kuwa ‘mpango’ au ‘msichana’ sio chakula likichopikwa ili kirejelewe kama kilichoiva. Mbinu hii ya utoaji wa kauli finyu hulenga kuafikia ufaafu kwa kuwa msikilizaji atatumia juhudi kidogo kuufikia umaanisho wanavyokariri Sperber na Wilson (2004). Hivi ni baadhi ya vitenzi ambavyo maana zake zimebadilika kwa kuhamisha, kupanua au kufinya maana na matokeo yake yakawa ni kwamba

usimbaji maana unazua umaanisho. Katika kauli zilizo hapo juu kitenzi kuiva kimepanuliwa kimaana na kupata maana mpya ya kukamilika au kukomaa.

Kitenzi ‘buna’ kinamaanisha ‘vunja.’ Hivyo basi, ‘kobuna’ ni ‘kuvunja’. Katika mazungumzo mtu atasikika akisema

30. *Enyomba eria yabunirwe*

Nyumba ile imevunjwa.

Hii ni tafsiri ya moja kwa moja. Kimazungumzo msemaji ni lazima awe na fahamu za awali za utamaduni zinazohusu ujenzi na ukamilishaji wa nyumba ili kupata fasiri sahihi. Kauli hii inaweza kuzua uwazi kwamba nyumba inayozungumziwa imevamiwa na wezi ambao huenda waliiba mali kutoka kwa nyumba hiyo. Kiumaanisho, kauli hii ina maana kwamba nyumba inayozungumziwa imekamilika ambapo mwenye nyumba ile anawahusisha jamaa zake, kwenye sherehe ndogo, na shughuli za mwisho mwisho za ujenzi, hasa kukamilisha uezekaji wa paa unafanywa. Fahamu za awali za tamaduni zinaelekeza ufafanuzi na uelewa wa tamko hilo.

### 3.4 Kategoria za Kimuktadha za Kiswahili na Ekegusii

Kategoria za kimuktadha tulizochunguza ni pamoja na mbinu za lugha pamoja na tamathali za usemi. Katika mbinu za lugha tulichunguza baadhi ya methali na nahau, ilhali tamathali za usemi tulizochunguza ni baadhi ya tashibihi, taashira na sitiari. Mbinu za lugha zimeelezwa kwa njia tofauti tofauti na waandishi

mbalimbali. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa: "Methali ni tamko lenye kueleza wazo la busara la binadamu kwa ufupi sana. Inaweza kusemwa kuwa ni muhtasari wa wazo la busara kwa mkato." Naye Wamitila (2001) anasema kuwa, "Methali ni usemi unaodhaniwa kuwa na ukweli ambao huwa na maana iliyofumbwa isiyoelezeka kwa maneno yaliyotumika katika usemi huo."

Methali ni usemi kamili unaoeleza dhana fulani ili kutathmini mahusiano ya kijamii, kueleza tajiriba ya maisha, kuwaadibu watu ama kutoa maonyo. Kutokana na maelezo haya, tunaweza kusema kuwa katika muktadha wa Kiswahili na Ekegusii, methali ni kauli za busara zenye maana iliyosimbwa kwenye maneno yaliyotumika na ambazo hueleza tajiriba za kimaisha pamoja na maadili ya jamii kwa kudai kuwa hali fulani ni ya kweli. Methali huwa na upekee kwa vile zina virai thabiti vyenye maana thabiti zisizobadilikabadilika, (Wamitila, 2001). Ingawaje, methali hubainika kama zinazozingatia tamaduni za jamii lugha zinamotumika kwa vile zinaelekezwa na utamaduni wa jamii hizo, lakini kuna methali sawia nazo katika lugha nyingine. Zinapotumika, matumizi ya methali hulenga urejelezi wa miktadha mingine ili kufikia ufaafu katika miktadha mahususi.

### 3.4.1 Methali za Kiswahili na za Ekegusii

Methali za lugha hizi mbili huonekana kuwa na utata mwingi zinapochukuliwa kwa maana za juujuu. Kwa mfano katika muktadha wa kazi ya kikoa, yule mwenyeji atasikika akisema kuwa:

31. Wawili si mmoja.

Wamitila (2001) na Arege & Nyanje (2011) wanasema kuwa methali hii inafananishwa na ile isemayo ‘umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.’ Methali hii inaibua hisia chanya za kuwahimiza watu kufanya mambo au kazi kwa ushirikiano kinyume na kujitenga. Ni muhimu kuzingatia muktadha wa mazungumzo panapozuka methali hii kwa vile kuichunguza kisemantiki kunadhihirisha utata. Methali sawia nayo katika lugha ya Ekegusii ni:

32. *Abange n’ baya bakaria ekiane nkaigwa bororo*.

Wengi ni wazuri, (lakini) walikula changu nikahisi uchungu.

Methali hii imegawanywa sehemu mbili, sehemu yenye wazo chanya na sehemu ya pili ina wazo hasi. Hata hivyo, kimsingi, inahimiza umuhimu wa ushirika, kwamba ingawa watu wengi watakula chakula kingi, pia wanafanya kazi nyingi na hivyo uzuri au faida inayotokana na ushirikiano inazidi matumizi yanayozuka.

Jambo lingine linaloibuka katika muundo wa methali hizi za lugha hizi mbili ni uchache wa maneno, kinyume na maelezo ya mazungumzo ya kawaida. Finnegan (1983) anaeleza kwamba methali za Kibantu zina utaratibu unaozingatia ubanifu ambapo mara nyingi kiima katika sentensi kinaachwa kwenye tamko lakini bado maana ikaeleweka. Iwapo methali hizi zingeandikwa kwa maelezo kamili zingekuwa:

(Watu) wawili si (mtu) mmoja.

*(Abanto) abange nabaya bakaria (egento) kiane nkaigwa bororo*.

(Watu) wengi ni wazuri walikuwa (kitu) changu nikahisi uchungu.

Aidha kwa kuzingatia kanuni ya upole (Leech 1983), methali ya Ekegusii inatumia njeo iliyopita kwa kuzingatia kanuni ya staha na kanuni ya majigambo ili kupunguza hisia za kuwadunisha wahusika pamoja na kupunguza majisifu. Katika hali ya kuonyesha kujitweza, wakati mwingi msemaji atatamka sehemu ya kwanza pekee ya methali hii '*bange n'baya*' na bado akaeleweka. Uwezo wa kuzifikia maana za methali hizi unatokana na uelewa wa muktadha, ambao unarejelea ushirika katika kufanya kazi. Msikilizaji anaelekezwa na muktadha kwenye ufaafu wa ujumbe ambapo anaafikia umaanisho kwamba uwezo wa watu wengi una thamani zaidi kuliko mtu mmoja au watu wachache ingawa methali zenyewe hazitaji nomino mtu. Hebu tuitathmini methali hii;

33. Mwana wa ndugu kirugu, mjukuu ni mwanangwa.

Kirugu ni sehemu ya mwili iliyovimba kama vile kipele au jipu. Mwanangwa ni mtoto wa watu wengine ambaye hamhusu mtu. Methali hii hutumika kuonyesha kuwa mtoto wa ndugu wa karibu hushughulikiwa kama vile mtu ajishughulishavyo anapokuwa na jipu mwilini mwake ilhali mjukuu huwa ni wa mbali na hivyo hamshughulishi sana mtu, (Arege 2011). Ili kufikia fasiri ya kauli hii, msikilizaji ni lazima awe na uelewa wa majina ya mahusiano ya watu katika jamii na ukoo ili kubainisha anachonuia mtoaji wa methali hii. Anapoelewa tofauti iliyoko baina ya mwana wa ndugu, mjukuu na mwanangwa pamoja na kirugu basi atahusisha kauli hiyo na muktadha ili kuafikia ujumbe ambao ungeweza kufupishwa kwamba kuna thamani zaidi kwa mtu au ndugu wa karibu kuliko yule

wa mbali. Methali ya Ekegusii yenye maana sawia na hiyo katika Ekegusii ni kama ifuatavyo:

34. *Omwana obande 'mamiria makendu*

(Mwana wa mwenyewe ni kamasi baridi).

Mtoto wa mtu mwingine ni kama kamasi baridi. Fasiri mbili zinaibuka kutokana na kauli hii. Uhusiano unamwezesha mpokezi wa tamko hili kuchuja maana ya msemaji kutokana na muktadha wa mazungumzo. Kwanza kabisa, mtu anapotamka methali hii huwa anaashiria hali ya kinyaa au kuchukizwa kutokana na dhana ya *'amamiria'* kamasi, na sio kamasi tu bali ni kamasi baridi. Methali hii hutumika na wanajamii, hasa wanawake kurejelea ukosefu wa shukrani kwa watu hasa watoto waliowasaidia na baadaye watoto hao wakakosa shukrani. Vilevile, methali hii huwa inarejelea jinsi wanawake huwatendea watoto wa jamaa zao hasa ikiwa mtoto ameachwa yatima na ikalazimu alelewe na mwanamke mwingine au mana wa kambo. Mazungumzo ya kila siku mara nyingi miongoni mwa wanajamii huwa ni kuhusu watu wengine, na mara nyingi mada huibuka hasa kuhusu mambo hasi katika jamii ambapo wazungumzaji hujadili tabia, matendo na maadili ya watu wengine (Dijk, 2008). Hivyo, methali hii haiwezi kuibuka tu pasipo kumrejelea mtoto fulani ambaye amekosa shukrani kwa mlezi wake, au mtoto yatima anayeteswa na mana wa kambo au jamaa yake.

Ufahamu na fasiri sahihi ya methali hii unabainika wazi kutokana na misamiati iliyotumika pamoja na muktadha. Zaidi ya hayo, mpokezi anatumia faliwa ya

kuona na kuhisi hasa kupata lengo la mtoaji kwenye neno ‘kamasi’ linalomletea mtu hisia za kukirihiwa.

Methali hizi mbili zinabainisha tofauti za mirengo na miyazamo ya kijamii. Katika lugha ya Kiswahili, mtoto wa ndugu ambaye anamhusu mtu fulani moja kwa moja hushughulikiwa zaidi kuliko yule wa mbali ambaye hamhusu mtu moja kwa moja, ingawa hadharauliwi.Hali hii ni tofauti  katika jamii ya Abagusii ambapo mtoto anayelelewa na mtu ambaye si mzazi wake halisi anachorwa kama anayedharauliwa, kubaguliwa na kutengwa na wazawa wa nyumba anamolelewa.Methali hii pia inadhihirisha ukosefu wa takrima, kuonyesha kuwa jamii ina mitazamo hasi kuhusu malezi ya mtoto ambaye si wa mtu halisi, na mitazamo ya jamii kuhusu watoto wa kambo. Methali nyingine inayobainisha tofauti za kimaana ni hii ifuatayo:

35. Mbwa koko mgeni kwa kila nyumba.

Methali hii pamoja na methali nyingine zinazohusu mbwa zinachora mbwa kwa njia chanya ambapo watu walio na tabia ya kusemasema sana (kubweka) na kutembea ovyo (mbwa koko) wanaonekana kama wanaokosa kutunzwa, yaani kukosa msimamo. Katika methali hii, mtu asiye na msimamo huonywa ili atulie katika maamuzi anayofanya. (Arege, 2011). Methali hii inaweza kupewa fasiri ya juujuu pia kwa kuwaelekeza watu kuchukua majukumu yao na kuwajibika na kuwatunza watoto na wanyama wao wasije wakawa kero kwa watu wengine kwa kwenda kudoea chakula kwa kila nyumba. Katika lugha za Kibantu, mbwa

anachukuliwa kama mnyama mchafu na asiyetamanika (Farsi 1973). Tazama methali

36. *Esese embe n'ya ngori 'ntambe*.

Mbwa mbaya ni wa kamba ndefu.(Hii ni fasiri ya kijuujuu).

Maarifa ya kiufasiri yanamwelekeza mpokezi wa kauli hii kwenye maana kusudiwa. Maana hiyo pia inaathiriwa na fahamu za awali za kitamaduni. Katika jamii ya Abagusii kuna chukulizi kwamba mbwa hufungwa na iwapo mbwa huyo atakata kile kifungo anaweza kwenda kuzurura akiwa na ile kamba yake shingoni, na kawaida mbwa wazururaji wanachukuliwa kuwa ndio hula kuku wa majirani na kuwashtua watoto wadogo. Fasiri ya methali hii ni kwamba mtu mwenye tabia mbaya, hata aende wapi, mbali au karibu, bado atadhihirisha tabia zake mbaya, hivyo hata ile kamba iwe ndefu, yaani aende masafa marefu, tabia yake haitabadilika. Vile vile, methali hii inanuia kuwaonya watu dhidi ya wanajamii wenye tabia na mienendo isiyoambatana na maadili ya jamii kama vile wizi, uzembe, na uchafu na hali ya kutojishughulikia kimaisha.

Katika methali hizi, tunaona kuwa ingawa methali zote zinazungumzia mbwa, uteuzi wa viarifu pamoja na jumbe zinazosimbwa zinatofautiana pia. Kutegemea mitazamo ya jamii hizi mbili, kuhusu mbwa, methali hizo zinazua umaanisho kwa kutumia mbinu ya uhamishaji ambapo binadamu analinganishwa na mbwa na hivyo msikilizaji akibadilisha neno mbwa na kutia mtu ataafikia maana ya methali hiyo kwa kutumia mbinu ya ulinganishi (Sperber & Wilson, 2004). Maana sahihi

ya kauli hii kiumaanisho inaweza kufikiwa iwapo mpokezi anaujuzi wa kiufasiri ili atumie juhudi kidogo zaidi kufikia umaanisho uliokusudiwa. Ujuzi huo pamoja na uhusiano wa ujube unaopitishwa utamwezesha kupata fasiri sahihi kutegemea muktadha wa mazungumzo.

37. Ng'ombe wa maskini hazai mapacha.

Maana ya methali hii ni kwamba ng'ombe wa mtu asiye na uwezo hazai mapacha, kwami akizaa mapacha umasikini utaisha na hivyo hatakuwa masikini tena, kwa sababu utakuwa na ng'ombe wengi kwa wakati mmoja. Fasiri ya methali hii inafikiwa na mpokezi wa kauli kwamba mtu mwenye uwezo duni hanyookewi na mambo. (Wamitila, 200 ; Arege na Nyanje, 2011) muktadha unaelekeza maana inayokusudiwa na msemaji.

38. *Eng'ombe ya bande 'mogoroba egoosia*

Ng'ombe wa mwenyewe hukata maziwa/hukauka jioni

Kauli hii inarejelea hali ambapo mtu aliyeazimwa kitu anaweza kupokonywa kitu hicho wakati ambapo hatarajii. Kutokana na fahamu za awali za awali za tamaduni, washiriki wa mazungumzo huelewa kuwa mtu anaweza kumpa jamaa yake ng'ombe amtunzie hadi wakati ambapo ng'ombe huyo atazaa. Bila shaka ng'ombe akishazaa, huanza kukamuliwa. Hata hivyo, si ajabu mwenye ng'ombe ajuapo kuwa ng'ombe wake amezaa, na anakamuliwa, ataenda na kumchukua bila arifa yoyote kwa yule jamaa wake, aliyemtunza kwa muda mrefu. Kwa jamaa aliyetegemea kufaidi na maziwa ya ng'ombe wa mwenyewe, ng'ombe huyo anapochukuliwa hutukia kama aliyekata au kukauka maziwa ghafla. Hivyo basi,

tamko hili katika muktadha kama huo likiunganishwa na fahamu za matukuo yanayozungumziwa huelekeza kwenye mahitimisho sahihi ya kile kilichokusudiwa na msemaji wa kauli, kwamba kitu cha kuazimwa hakikidhi mahitaji ya mtu, sawa na chake. Methali ya Kiswahili yenye maana sawa na hiyo ni :

Nguo ya kuazima haisitiri matako.

Methali hii ina maana kwamba, kitu chama tu mwingine, hata kiwe kizuri au chenye manufaa vipi, hakiwezi kukidhi haja zote za yule aliyekiazima, kwa vile huenda akanyanganywa kitu hicho au kuaibishwa wakati asipotarajia. Methali mbili zinazozua umaanisho kuhusiana na ng'ombe katika lugha hizi mbili zina maana mbili tofauti kabisa na hivyo haziwezi kutumika katika miktadha inayofanana.

Katika mazungumzo ya kawaida kati ya wanajamii wawili, mmoja anaweza kusikika akisema :

39. *Susana n'Okong'o nyamenwa ebere*

Susana ni Okong'o mwenye midomo miwili.

Kauli hii kwenye maana mbili, uwazi na umaanisho. Maana kiuwazi ni kwamba Susan ana sifa za Okong'o anayejulikana kutokana na fahamu za awali za kitamaduni kwa kutokuwa na msimano. Maana ya msemaji inafikiwa kwa kutumia mbinu ya uhamishaji wa sifa ya mtu aliyejulikana na kumpa mtu mwingine sifa hiy. Maana kiumaanisho inaelekezwa na maarifa ya kiufasiri, kwamba Susana ni

mchonganishi, kwamba anapeleka umbeya kwa watu wawili tofauti kwa makusudi ya kuwachochea wagombane. Methali hii inaweza kulinganishwa na nahau ya kiswahili kwamba :

Susana ni ndumakuwili.

40. *Ge'koboko nke'monwa are*

Kilicho mkononi kiko mbali na mdomo.

Katika kauli hii, kiuwazi msemaji anamaanisha kwamba chakula alichokimega mtu kwa mkono si lazima akitie mdomoni kwa vile huenda kikamponyoka na hivyo kukosa kutiwa mdomoni. Ufahamu huu unatokana na udokezaji wa msemaji pamoja na muktadha wa mazungumzo. Fasiri hii ni ya uwazi. Fasiri ya kimaarifa inayomwelekeza mpokezi kufikia maana ya kauli hii ni kwamba jambo linaweza kuonekana kama lililokamilika na kutengemaa lakini kumbe kunaweza kuzuka hali ya kukinza matilaba ya jambo hilo. Methali sawia na hiyo ni :

Kutangulia si kufika.

### 3.4.2 Nahau

Katika mazungumzo ya kijamii, nahau zimeonekana na kuchukua nafasi kubwa sana, kwanza kama mbinu ya kimawasiliano na pili kuirembesha lugha (Farsi 1973). Dhana zinazoeleweka katika mazingira ndizo hutumika na maana dhana hizo huhamishwa na kuwekwa kwenye miktadha mahususi na wazungumzaji kwa matilaba maalum (Stamenkovic, 2010). Ijapokuwa nahau hubainika kama kifungu cha maneno chenye kitenzi na maneno mengine ya kileksika, nahau huwa na

maana moja, na wakati wowote mtu akijaribu kuvunja au kuyatenga maneno kwenye nahau maana ya nahau hizo hupotea Kiango (2000). Maana msingi za vitenzi au nomino huhamishwa na kupata maana mpya ya kimazungumzo ambazo wazumgumzaji hutumia kuafikia malengo yao (Ullman, 1970).

Kauli ifuatayo pia inazua uwazi na umaanisho:

41. *Chibesa chiane nigo <u>chianywa amache</u>*

Pesa zangu <u>zilikunywa maji</u>

Udokezaji unaotokana na kauli hii ni kwamba pesa zilirowa maji na hivyo haziwezi kutumika tena. Hata hivyo, mpokezi na mnenaji wakiwa katika ngazi moja, umaanisho unaokusudiwa ni kwamba pesa zangu zilipotea bure! Mzungumzaji anaashiria kuwa alipata hasara kwa shughuli iliyolenga faida au manufaa fulani. Nahau sawia na hii katika lugha ya kiswahili ni ‘kuambulia patupu’.

‘*Gochia nyomba’* ni kirai chenye maana ya ‘kuingia au kuelekea kwa nyumba’.

Katika kauli ifuatayo, maana tofauti zinaibuka :

42. *Maranga n’oNyamweya <u>achiete nyomba</u>*

Uwazi wa kauli hii ni kwamba Maranga ameingia ndani ya nyumba ya Nyamweya. Umaanisho wa tamko hilo ni kwamba Maranga amesuhubinana na mke wa Nyamweya licha ya kwamba yeye ni mume aliye na kwake na ana mke. Hali kama hii hutokea hasa mtu anapokufa na kumwacha mke ambaye baadaye

hurithiwa, yaani '*gochiegwa nyomba'* na mtu mwingine. Matumizi ya kauli hii yenye umaanisho badala ya uwazi yanoongozwa na kanuni ya upole na fahamu za tamaduni zinazomtumikiza lugha kimafumbo (Leech, 1983 ; Yule, 1986 ; Sperber & Wilson, 1986).

### 3.4.3 Nahau za Kiswahili

Nahau ni mbinu ya lugha ambayo hutumika sana katika mazungumzo ya kawaida. Katika lugha ya Kiswahili kama inavyobainika katika lugha nyinginezo nahau hutumika katika mazungumzo rasmi na yasiyo rasmi pamoja na misimu. Nahau hutumiwa sana na washairi. Maandishi ya dini pia hutumikiza nahau kwa wingi. Nahau za Kiswahili zinapotumika katika mazungumzo au hata katika maandishi huzua umaanisho kinyume na uwazi ambao utaelezwa kutokana na maana msingi ya maneno yalitumiwa kama:

43. Baba yake aliaga dunia miaka mitatu iliyopita.

44. Manusura wa ajali ya moto amekata kamba.

45. Jambazi yule ametupa mkono baada ya kupigwa risasi na polisi.

Katika kauli za 40, 41 na 42 nahau zilizopigwa msitari zina maana moja ambayo ni 'kufa.' Hata hivyo katika mazungumzo, watu hukwepa kutumia neno 'kufa' moja kwa moja kwa sababu katika tamaduni nyingi kutaja kifo moja kwa moja ni mwiko. Vilevile, majina yanayohusiana na sehemu za siri, uzazi na nguo za ndani; majina ya Mungu, pamoja na kutaja majina ya wanyama fulani hasa wakati wa

usiku huwa haifanywi wazi wazi au hadharani. Hali hii ndiyo huelekeza watu wakasikika katika mazungumzo wakisema:

46. Jane ameenda haja

47. Julia ni mja mzito.

Kauli ya (43) inamaanisha kwamba Jane ameenda msalani ilhali ya (44) in maana kwamba Julia ana mimba. Katika kuyatumia maneno yaliyosimbwa na nahau hizo moja kwa moja jamii zinaamini kwamba maneno hayo yanaweza kumtia mtu unajisi mtumizi wake au hata msikilizaji wake na hivyo kuzifisidi akili zao na watu wengine kwa jumla. (Wilson 1967).

Nahau nyingine zimeundwa kutokana na matumizi ya majina ya vitu nau nomino halisi na za kidhahania ili kuwakilisha vitu halisi. Katika lugha ya Kiswahili nomino ‘damu’ imetumika kuunda nahau kama vile:

48. Damu ya Mwafrika ilimwagika wakati wa ukoloni.

49. Mtoto huyu ni damu yetu.

Katika nahau hizo, ‘damu’ katika kauli ya (45) inamaanisha kuwa Waafrika wengi walikufa wakati wa ukoloni na wala sio damu halisi iliyotiririka kama maji. Fasiri hii inatokana na imani za kitamaduni kwamba kumwagika kwa damu husababisha kifo. Katika kauli ya (46) ‘damu’ imetumika kuashiria uhusiano wa kiukoo kwa kuwa watu wa koo moja wanaaminika kutoka kwa kizazi kimoja na kuwa na mahusiano ya kijamaa.

Ufahamu wa mila, tamaduni na itikadi za watu pamoja na miktadha ya mazungumzo ndiyo kigezo kikubwa katika kuelekeza fasiri ya nahau katika lugha ya Kiswahili. Aidha nahau zinatumika sawa kimazungumzo ijapokuwa maana yazo huwa sio ya moja kwa moja kwa kuwa fasiri za kileksika haziafikii maana za nahau hizo, ambazo lengo lake ni umaanisho dhidi ya uwazi (Hurford & Hearsley, 1983).

### 3.4.4 Nahau za Ekegusii

Nahau ni sehemu kuu ya lugha ya mazungumzo miongoni mwa matumizi ya lugha yakiwemo yale ya lugha ya Ekegusii. Kama nahau za Kiswahili, nahau za Ekegusii zina muundo wa nomino na kivumishi, kitenzi na nomino, kama nahau :

*Gotwa amate*

(Kutema mate)

Nahau hii ina maana nyingi kiumaanisho kutegemea, miktadha ingawa kiuwazi inamaanisha ‘kutema mate.’ Maana za kileksika za kitenzi na nomino zinazounda nahau hii zinahamishwa na kuunda dhana moja ambayo huzua maana kadhaa katika miktadha tofautitofauti. Kauli kadhaa zenye nahau ‘gotwa amate’ zinaweza kuzua maana tofatutofauti kutegemea miktadha zinapotumika. Tazama mifano ya kauli :

50. *Mondetere abachokoro bane <u>n’batwere amate</u>.*

Mniletee wajukuu wangu niwatemee mate.

51. *Tiga n'ragenda gotwa amate.*

Hebu niende kutema mate.

52. *Ntwaeta bw'omosubati otoa 'gento twatwera 'mate inse.*

Tulipitia kwa dada yetu akatupa kitu tukatema mate chini.

53. *Ekero ngogotebia okore emeremo nigo ogontwera amate.*

Ninapokwambia ufanye kazi huwa unanitemea mate.

Katika kauli hizo zote, nahau 'gotwa amate' yaani kutema mate inazua umaanisho, kila mmoja akiwa tofauti na ule mwingine. Katika tamko la (47) umaanisho unaozuka ni kuwa msemaji anaomba aletewe wajukuu wake ili awabariki. Uwezo huu wa kubariki unaelezwa na Austin (1962) katika Thomas (1995) kuwa kuna vitendo ambavyo hutekelezwa kwa kutumia lugha pekee.

Kauli ya pili inazingatia uhamishaji wa maana za kileksika za '*gotwa amate'* kutema mate ambapo maana inayoibuliwa ni kwenda kujisaidia. Uhamishaji huu wa maana unazingatiwa kwa sababu za kanuni ya upole pamoja na tamaduni zinazoelekeza matumizi ya lugha inayozingatia utaratibu chanya, (Leech, 1983). Tamko hili linapotolewa linazua matarajio ya uhusiano na ufaafu kwa sababu msemaji anatarajiwa kuzingatia kanuni ya ushirikiano, pamoja na uwezo wao wa kiufahamu ambao anatarajiwa kutumikiza, yeye na msikilizaji wake. (Sperber & Wilson 2004). Muktadha una jukumu kubwa pia katika hali ya kuwezesha kuifikia fasiri sahihi ya kauli hizi.

Uwazi wa kauli ya (50) ni kwamba 'tulipitia kwa dada yetu akatupatia kitu tukatema mate chini.' Katika jamii hii, '*omosubati*' ni dada ambaye ameolewa. Kauli hii inaibua matarajio ambayo yanamwelekeza msikilizaji kuifikia maana ya msemaji, kwamba iwapo msemaji alipita kwa dada yake, basi kinachotarajiwa kando na mambo mengine ni kupewa chakula.

Hivyo basi, hiki kinachoitwa *'gento'* au kitu ni chakula, na kutema mate '*gotwa amate'* ni kula na kunywa. Hata hivyo, katika kauli hi, nahau '*gotwa amate'* inabeba kiwango fulani cha ukanushaji – hali ya kuonyesha kuwa ingawa walipewa chakula, kilikuwa kidogo tu cha kuwatuliza ili waweze kuendelea na safari yao.

Katika kauli ya 31) msemaji anatoa kauli inayozua umaanisho kwamba mpokezi anayapuuza yale anayoambiwa. Hali hii inatoka na tabia na mazoea ya kijamii kwamba kutema mate ni ishara ya kuonyesha hali ya kudunisha au kulidharau jambo. Fasiri hii inafikiwa na huwa inaeleweka na maarifa ya awali ya kitamaduni katika mazungumzo ya ana kwa ana, na ambayo huelekeza tabia za watu wa jamii moja. (Yule, 1996). Tazama kauli nyingine:

54. *Tata omwabo orarire*

55. *Omwana bw'Osoro osirire*

56. *Bwamwabo natonyoora*

Katika kauli hizi, ulinganishi wa moja kwa moja na nahau za Kiswahili zinazozua maana ya kufa unatofautiana pakubwa kwa vile hizi za Ekegusii zinatumia kitenzi kimoja kinachozua maana ile ile moja ya kufa. Tunaona katika sehemu ya 3.5 jinsi vitenzi hutumika kuzua umaanisho katika mazungumzo. Maana msingi ya vitenzi hivyo ni kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *Rara* | *orarire* | amelala |
| *Sira* | *osirire* | amepotea |
| *Nyoora* | *otonyorire* | ametuacha |

Kuna maana nyingine zaidi ya fasiri '*orarire*' yaani amekufa inayoibuliwa na vitenzi hivi. Vitenzi hivi vinaibua hisia tofauti tofauti, zikiwemo hali ya kupumzika – mtu anapolala, hali ya kusikitisha mtu anapopotea na hali ya huzuni na majonzi mtu anapoachana na jamaa zake wakielewa kuwa hawataonana tena. Hivyo kuna umaanisho mara mbili, kimaana na kihisia.

Katika jamii ya Abagusii, kumwaga damu ni dhana inayoashiria mauaji, kisasi au mwiko. Hivyo basi, katika kauli:

57. *Goitera amanyinga*

Kumwaga damu

Inaweza kuzua maana hizo tatu. Aidha mtu akisema.

Intwe *namanyinga ayamo* (sisi ni damu moja) anamaanisha kuwa wao ni watu wa ukoo mmoja, sawia na kauli hiyo hiyo katika lugha ya Kiswahili. Umaanisho unaoafikiwa kutokana na kuuelewa muktadha pamoja na ufaafu wa pembejeo

inayotumiwa na msemaji na ambayo ni muhimu kwa kwa msikilizajji wake (Sperber na Wilson, 2004).

### 3.4.5 Tamathali za Usemi

Katika sehemu hii, baadhi ya tamathali za usemi zikiwemo tashibihi, taashira pamoja na sitiari zimejadiliwa. Tamathali hizo zikichukuliwa kwa uwazi wake zinazua utata, na hiyo ndiyo sababu ni lazima msikilizaji amakinike kwa kupambanua umaanisho wazo kusudi apate maana ya msemaji.

### 3.4.6 Tashibihi

Kuhenga (1977) anaeleza kuwa: "Tashbihi limezaliwa kutoka kwenye neno 'shabihi'. Kushabihi maana yake kufana au kulingana na, kuwa sawasawa na au kulanda'. Tofauti na sitiari, tashbihi, hutumia mbinu ya ulinganishaji kwa viunganishi 'kama,' 'ja,' 'mithili ya,' na 'mfano wa'. (Wamitila, 2003). Viunganishi hivyo hutumika kwenye tashibihi katika lugha ya Kiswahili na katika Ekegusii. Kiunganishi kinachotumika sana kulinganisha vitu katika lugha ya Ekegusii ni '*buna*' (kama) na '*-nga buna*' 'ni sawa na'.Tazama mifano hii:

58. a) Baba yake ni <u>mkali kama simba</u>, ni sawa na

    b) *Tata omwabo <u>n'omotiridi buna endo</u>*.

59. a) Mtu Yule ni <u>mweusi kama makaa</u> inaweza kulinganishwa na

    b) *Omonto oria <u>n'omomwamu buna embiro/egusunte.</u>* '*Embiro*' inarejelea masizi. Pia mtu yule ni <u>mweusi kama giza</u>.

60. a) Darasa lilinyamaza kama kaburi ni sawa na

b) *Aborokigwa rigo baakirete buna enyasi* (wanafunzi walinyamaza kama ukuta).

Tazama mfano mwingine wa tashibihi ya Ekegusii

61. *Ayoti n'omweng'e buna egetugi*

Ayoti ni mfupi kama kisiki

Katika tashibihi hii, Ayoti ambaye ana kimo kidogo anafananishwa moja kwa moja na kisiki. Kutokana na fahamu za awali kuhusu kisiki, mpokezi wa kauli hii anaelekezwa kwenye ujumbe wenye msisitizo, kwamba mrejelewa ni mtu mfupi sana. Uelekezi huu unamsaidia kutumia juhudi kidogo zaidi kuifikia maana ya msemaji. Tashbihi inayorejelea ufupi katika lugha ya Kiswahili ni

Ayoti ni mfupi kama nyundo.

Uteuzi wa vitie vinavyorejelea dhana ya ufupi unatofautiana katika lugha hizi mbili kutokana na tofauti za tamaduni na mazingira. Katika Kiswahili, kitu kifupi zaidi ni nyundo ilhalli katika Ekegusii kitu kifupi zaidi ni kisiki.

Jamii hizi mbili zinatofautiana katika kulinganisha vitu vyenye kimya. Katika Kiswahili, ni mwafaka zaidi kueleza kimya kwa kulinganisha na muktadha wa kaburi ilhali katika Ekegusii ukuta ndio unafananishwa na hali ya kutokuwa na kelele yoyote. Aidha, ukwepaji wa matumizi ya kaburi unatokana na imani za kutotamka kaburi waziwazi, kwa vile ni mwiko kusemasema mambo yanayohusiana na kifo.

Lengo kuu la matumizi ya tashbihi kimazungumzo katika lugha zote mbili ni kuleta mitagusano ya kimawazo ya juhudi na matokeo ambapo dhana moja inapewa sifa za dhana nyingine na hivyo kuepuka maelezo mengi. (Sperber & Wilson, 2004).

**3.4.7 Taashira**

Kamusi ya TUKI (2004) inasema kuwa: 'Taashira ni ishara au dalili'. Katika mazungumzo, ishara au vitu vinavyowakilisha dhana fulani hutumiwa badala ya maelezo marefu kuhusu dhana hizo. Ishara hizo huwa zinaeleweka kutokana na ufahamu wa kitamaduni wa watumizi wake na hivyo hueleweka kwa njia rahisi kwa wale walio na ufahamu huo (Yule, 1996). Kwa mfano, ishara moja inaweza kutumiwa katika lugha ya Kiswahili na Ekegusii kuzua umaanisho ule ule. Tazama mifano hii:

62. a) Yohana amepewa bendera.

    b*) Yohana  n'aegwa ebendera*.

63. a) Fimbo humrudi mtoto mtukutu

    *b) Enyimbo nero ekogorora omwana omokarakari*.

64. a) Naona umeota mvi.

    b) *N'roche kwamerire chimbuche*.

65. *Aborokia babekire echoka inse*

    Walimu wameweka chaki chini.

Katika kauli hii, chaki ni taashira inayowakilisha taaluma ya ualimu. Fasiri inayoweza kutolewa kutokana na kauli hii ni kwamba walimu wamesitisha kazi ya kufundisha kutokana na sababu fulani. Kando na ukweli kwamba chaki ni kifaa muhimu cha kazi ya ufundishaji, maana yake kimazungumzo inapanuliwa na hivyo kuzua umaanisho wa shughuli nzima au kazi ya kufundisha. Hivyo basi, mpokezi wa kauli hii anaelekezwa kwenye fasiri kwamba walimu wamegoma kutokana na kirai 'kuweka chaki chini.'

Tazama taashira nyingine:

66. *Mwa Mokaya y'okire* <u>*omorero*</u>

Kwa Mokaya kumewaka <u>moto</u>

Moto ni taashira inayoweza kutumiwa kuzua maana kadhaa kiuwazi, na kauli hiyo ina maana kwamba 'nyumba ya Mokaya inachomeka'. Hata hivyo kiumaanisho, mzungumzaji anasisitiza wazo kwamba kwa Mokaya kuna vita, au ugomvi. Taashira ya moto inaelekeza kwenye msisitizo kwa kuihusisha kauli hiyo na ufahamu wa awali kuhusu kile kinachozungumziwa ili kupata umaanisho. Mpokezi wa kauli hii anaelekezwa kuteua maana inayofaa na inayomwelekeza kwenye ufaafu kulingana na muktadha wa wakati huo.

Taashira zilizopigiwa mistari zimetumika kutamathali na wasemaji kwa kusudi la kuhusishwa katika mazungumzo pamoja na kuelekezwa kwenye jumbe muhimu zilizo katika matamko hayo. Mbinu inayotumiwa na wamemaji wa kauli hizo ni ile

ya upanuzi wa maana ambapo maneno yanapata maana nyingine za kisemantiki katika miktadha mipya (Ullman 1970) ambapo yanamaanisha dhana zifuatazo:

bendera - madaraka

fimbo - adhabu

mvi - umri mkubwa/uzee.

Uwezo huu wa maneno kupata maana mpya kitamathali unaweza kuelezwa kwa kutumia nadharia ya uhusiano ambapo jumbe zinazotolewa zina ufaafu kwa msikilizaji, pamoja na uwezo wa mpokezi kuzisimbua ni uwezo wa kimawasiliano ambao hutenda kazi katika mazungumzo.

### 3.4.8 Sitiari

Sitiari ni tamathali ya usemi yenye maana ya kuhusisha kitu kimoja na kingine chenye sifa zinazofanana. Hutumika kulinganisha dhana mbili bila kutumia maneno 'kama,' 'mithili ya,' 'ja' na 'kama vile.' Kitu kimoja kinaelezwa kana kwamba ni kingine. Ulinganishi huu ni wa moja kwa moja (Wamitila, 2003; TUKI, 2004). Katika lugha ya Ekegusii sawia na Kiswahili, sitiari hutumika kimazungumzo kusimba maana za dhana ambazo zingeelezwa kwa maneno mengi.

67. a) Ujana ni moshi.

b) *Obosaae n'erioki*.

68. a) Elimu ni utajiri.

b) *Chiseemi n'oboonda*.

69. Mvua ni shibe

*Embura n'omoigoto*

Sifa za dhana moja katika sitiari hizi zinahamishwa na kupewa dhana ya pili. Msemaji anakuwa na chukulizi kwamba msikilizaji anaelewa dhana ya pili na sifa zake ili kupata umaanisho aliokusudia, kwamba, kama vile moshi, ujana hudumu kwa muda kisha ukatoweka, elimu itampa mtu utajiri na kwamba mradi kuwe na mvua, basi watu hawakosi chakula kwani ndiyo husaidia kukua kwa mimea itumiwayo kama chakula. Sifa za kitu cha kwanza huchukuliwa kuwa sifa ya kitu cha pili kwa njia sisisi.

Fasiri ya sitiari katika lugha zote inafikiwa kwa kuhamisha sifa za dhana rejelewa kwenye dhana rejelezi na kufikia umaanisho katika mazungumzo. Sitiari zinaweza kutumiwa hata bila kuzingatia miktadha kwa kuwa ni kauli zenye maana za ubia. Tofauti zinazoweza kubainika ni za kitamaduni na kimazingira ambapo vitu vinavyolinganishwa huwa tofauti lakini sifa zake zinafanana.

### 3.5 Hitimisho

Katika sura hii uchanganuzi wa maana za kileksika za maneno na maana umaanisho za kategoria za kileksika na kategoria za kimuktadha umefanywa. Nadharia ya Uhusiano imeeleza jinsi jumbe humfikia msikilizaji na jinsi jumbe hizo hufasiriwa ili kupata kilichomaanishwa na msemaji ingawa hakikusemwa na neno au tamadhali ya usemi katika muktadha mahususi. Kwa misingi ya nadharia

ya uhusiano inaonyesha kwamba ujumbe unaopitishwa na msemaji huwa unaundwa kipragmatiki kuambatana na fahamu zinazoelekezwa na mbinu za kiuhusiano na ufaafu zenye chukulizi za kiurejelezi kutokana na dhana zilizosimbwa kwenye neno au tamathali ya semi, pamoja na maneno mengine kwenye sentensi nzima. Umaanisho unaofikiwa kwa kusimbua dhana zilizosimbwa kwenye maneno au tamathali zilizotumiwa na msemaji kama sehemu ya yaliyomo kwenye kauli huwa umezuiwa katika kila hatua, na utafutaji wa fasiri ndilo kusudi la msemaji, kwamba msikilizaji atambue alichomaanisha msemaji na hakukisema. Uwezo wa kiakili wa msikilizaji ndio utawezesha ufikiaji wa maana kutegemea juhudi zake, na iwapo atatumia juhudi kubwa zaidi kuufikia ujumbe, basi ujumbe wenyewe hauna ufaafu mkubwa kwa mpokezi. Muktadha wa muzungumzo huchangia pakubwa katika kuelekeza ufaafu kwa vile unatoa vidokezo kwenye jumbe muhimu katika mazungumzo.

Nadharia ya uhusiano hutenda kazi kwa kuzingatia kanuni mbili kuu. Kanuni ya kwanza inahusu ujuzi au uwezo wa mpokezi wa kauli kufasiri kilichosemwa kwa kutumia juhudi kidogo zaidi kupata maana iliyokusudiwa. Ujuzi huo hutokana na fahamu za awali za utamaduni pamoja na miktadha mnamotumika misimbo. Kanuni ya pili inahusu uhusiano wa ujumbe unaosemwa kwa msikilizaji. Ujumbe wenye umuhimu kwa msikilizaji una nafasi kubwa zaidi ya kupata fasiri sahihi kwa urahisi kuliko ujumbe usio na uhusiano mkubwa kwa mpokezi.

# SURA YA NNE

# MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inatoa mahitimisho kuhusiana na uchunguzi ambao ulilenga kulinganisha jinsi lugha za Kiswahili na Ekegusii zinavyotumia misimbo katika mazungumzo na kuzua umaanisho. Kategoria mbalimbali za kisemantiki zimechunguzwa. Kategoria za kwanza zilichunguzwa ni zile za kileksika ambapo uchunguzi huu ulishughulikia baadhi ya nomino na vitenzi pekee katika lugha zote mbili. Vilevile, baadhi ya mbinu za lugha pamoja na tamathali za semi ambazo huibuka kimazungumzo katika lugha hizo ulijadiliwa. Tamathali za lugha zilizochunguzwa ni tashibihi, taashira na istiari. Mbinu za lugha zilizochunguzwa ni methali na nahau. Ili kuifikia maana ya msemaji, Nadharia ya Uhusiano iliyoasisiwa na Sperber na Wilson ilitumiwa. Miktadha iliyotumiwa ni ya kijamii ambapo jamii iliyolengwa ni ya kundi la watu ambao wanaishi eneo moja, wenye utamaduni mmoja na huzungumza lugha moja na katika shughuli zao za siku na kila mara huwa na mitagusano. Katika sura ya pili na ya tatu, kategoria za kisemantiki zimejadiliwa kwa kutumia Nadharia ya Uhusiano na kufikia mahitimisho kadhaa.

## 4.2 Mahitimisho

Maana za kategoria za kisemantiki zilizochunguzwa imebainika kuwa inabadilika hasa kategoria hizo zinapotumika katika mazungumzo. Kategoria za kileksika katika lugha za Kiswahili na Ekegusii zimedhihirisha mshabaha mkubwa

zinapoelezewa bila miktadha. Hata hivyo, katika mazungumzo, kategoria hizo zimeonekana kutofautiana pakubwa ambapo maana za nomino au vitenzi zinabadilika na kupata maana nyingine tofauti na maana za kikamusi zinayojulikana katika lugha hizo mbili. Katika miktadha ile ile ya kijamii, lugha za Kiswahili na Ekegusii zimeonekana kuteua nomino au vitenzi tofauti tofauti kuwakilisha dhana moja. Hali hii inakanusha nadharia tete ya kwanza iliyokisia kwamba kategoria za kisemantiki zinazozua umaanisho katika lugha ya Ekegusii na Kiswahili zinafanana. Ijapokuwa lugha hizo zote ni za Kibantu na zina muundo wa maneno na muundo wa kisintaksia unaoshabihiana, nomino na vitenzi vilevile katika miktadha inayofanana vinapotumika kimazungumzo wakati mwingine huzua utata ambao ni mbinu ya kimawasiliano inayotumia uhusiano kufasiri maana hiyo na kufikia ujumbe uliokusudiwa na msemaji.

Matumizi ya tamathali za usemi zinazoelezea dhana moja zimebainisha tofauti kubwa pia katika lugha hizi mbili. Chukulizi za uwazi wa kauli za kitamadhali zimeonyesha kuwa maana ya msemaji haiwezi kuafikiwa kutokana na maana za maneno yaliyotumiwa. Hivyo basi, inabidi msikilizaji atumie ufahamu wa utamaduni na uwezo wake wa kiakili ili kufikia ufaafu wa jumbe zilizosimbwa kwenye kauli zenye tamathali za usemi. Aidha, kwa sababu tamathali hizo huwa zinazua utata, muktadha unachukua nafasi kubwa kufanikisha ufafanuzi sahihi wa kauli kwa kuzielekeza jumbe kwenye ufaafu. Wazungumzaji wa Kiswahili wanateua tamathali za semi kwa kuzingatia mitazamo ya kitamaduni, tofauti na

jinsi wazungumzaji wa Ekegusii wanavyoteua tamathali za semi katika lugha yao. Kutokana na hali hii, uteuzi wa maneno na tamathali za usemi zinazozua umaanisho kiusemi katika lugha hizi ni tofauti, na hivyo kukanusha ukweli huu, pamoja na tamaduni zilizochanyanuliwa nadharia tete ya kwanza iliyokisia kwamba kategoria za kisemantiki zinazozua umaanisho kimazungumzo katika lugha ya Ekegusii zinafanana na zile za lugha ya Kiswahili.

Tathmini ya maana za kileksika za kategoria za kisemantiki ambazo zinapotumika kimazungumzo kuzua umaanisho katika lugha ya Kiswahili na Ekegusii imeonyesha kuwa kuna tofauti kubwa za kiumaanisho na kategoria za kileksika katika lugha za Ekegusii na Kiswahili. Tofauti hizo zinaletwa na tofauti za kuifahamu za kitamaduni, matumizi ya mbinu ya upanuzi na uhamishaji wa maana za dhana kwa kuyapa maneno yaliyotumika kuelezea dhana fulani yanakanusha ile nadharia tete ya pili iliyokisia kwamba maana za kileksika za kategoria za kisemantiki zinazozua umaanisho kimazungumzo katika Ekegusii ni sawa na zile za Kiswahili.

Baada ya kuchanganua baadhi ya methali za Kiswahili na za Ekegusii zinazorejelea dhana moja, utafiti huu ulingundua kwamba hakuna methali katika lugha ya Ekegusii inashabihiana neno kwa neno na methali sawia nayo katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, lugha hizi zinatumia miundo tofautitofauti ya methali kuzua dhana za kimaana ambazo zinafanana au kukaribiana kimaana.

Hivyo basi, uteuzi wa methali itakayofaa kimazungumzo katika Kiswahili kwenye muktadha fulani ni tofauti na uteuzi wa methali ya lugha ya Ekegusii ambapo methali ya Ekegusii itakayotumika katika miktadha uleule itakuwa na uteuzi tofauti wa maneno pia ingawa maana zinaweza kuwa na uhusiano. Hali hii inabainika kutokana na jumbe zilizo katika methali za Kiswahili ambazo mara nyingi zina mielekeo chanya kinyume na methali za Ekegusii ambazo mara nyingi zina mielekeo hasi. Mbinu ya fasiri ya methali kwa kutumia nadharia ya uhusiano ni ile ya kutumia ufahamu wa kitamaduni, pamoja na kulenga ufaafu wake katika mazungumzo.

Uchunguzi wa nahau umebainisha kuwa miundo ya nahau za Kiswahili na zile za Ekegusii inafanana..Hata hivyo, hakuna nahau ya lugha moja inayolingana kimaana na nahau ya lugha nyingine, na kujaribu kufanya hivyo kunasababisha kupotea kwa maana ya nahau hiyo. Hali hii imebainika kati ya lugha za Kiswahili na Ekegusii ambapo uteuzi wa maneno yanayounda nahau hizo yanatofautiana licha ya kuwa zina maana moja. Maana za nahau pia inaeleweka kwa kutumia zile mbinu za kinadharia za uhusiano. Miundo ya nahau pamoja na umaanisho wake kimazungumzo inakinza nadharia tete ya kwanza katika utafiti huu.

Mlingano wa kimuundo na wa kimaana ulibainika katika tashbihi, taashira na istiari zinazotumika kimazungumzo katika lugha hizi mbili. Aidha, ufahamu wa ujumbe wa msemaji unarahisishwa na mbinu ya ulinganishi na ufananishi

unaotumika katika tamathali hizi. Mtu anapofananisha kitu na kingine katika mazungumzo anamshirikisha msikilizaji wake kutambua sifa za kitu cha pili ili apate ujumbe wa msemaji. Hivyo basi tunaweza kusema kwamba kategoria hizi za kimuktadha za lugha za Kiswahili na Ekegusii zimekubaliana na nadharia tete ya kwanza inayosema kwamba kategoria za kisemantiki zinazozua umaanisho kimazungumzo katika lugha ya Ekegusii na Kiswahili zinafanana.

Utafiti huu umedhihirisha kwamba ijapokuwa miktadha ya mazungumzo inaweza kuwa inafanana kati ya wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii na wale wa Kiswahili, tamaduni, imani mitazamo na mazingira ya jamii lugha huelekeza uteuzi na uundaji wa kauli zenye umaanisho kimazungumzo. Hivyo basi, miktadha pekee haiwezi kufanya uteuzi wa maneno yanayotumiwa kimazungumzo kufanana iwapo lugha mbili tofauti zitatumika. Uteuzi wa maneno au tamathali za usemi zenye umaanisho mazungumzo hutegemea umri, vyeo, matilaba na wahusika wengine waliomo katika mazungumzo. Hali hii inaelekea kuikanusha nadharia tete ya tatu inayosema kwamba miktadha ya matumizi ya kategoria za kisemantiki katika lugha za Ekegusii na Kiswahili inafanana. Utafiti huu umebainisha kwamba licha ya kwamba Kiswahili na Ekegusii ni lugha za Kibantu, uteuzi wa misimbo inayozua umaanisho kimazungumzo inatofautiana pakubwa kwa sababu ya tofauti za kimazingira, kiimani, kitamaduni na kimtazamo kati ya wazungumzaji asilia wa lugha hizi mbili.

## 4.3 Mapendekezo

Utatifi huu ulikusudia kuchunguza umaanisho unaozuka kimazungumzo kwa kutumia Nadharia ya Uhusiano. Uchunguzi huu haukushughulikia umaanisho unaozuka kutokana na kategoria nyingine za kisemantiki. Katika lugha hizi mbili, kategoria za kileksika kama vile vivumishi, vielezi na vihisishi havikushughulikiwa. Aidha, kategoria za kimuktadha kama vile, tasfida, nidaa, tabaini na nyinginezo hazikushughulikiwa. Hivyo, basi, kuna mengi yaliyobaki na yanayohitaji kutafitiwa katika kuchunguza kategoria nyingine za kisemantiki ambazo utafiti huu haukushughulikia. Aidha, kategoria zilizoshughulikiwa zinaweza kutafitiwa kwa kutumia nadharia nyingine ili kuonyesha jinsi fasiri sahihi za kauli zinaweza kufikiwa.

Katika uchanganuzi wa kinadharia wa kauli za kimazungumzo, vijenzi vingine vya kimazungumzo kama vile sauti, toni na ishara za uso hazikushughulikiwa ingawa zina jukumu kubwa katika mazungumzo ya ana kwa ana na hivyo zinahitaji tafiti nyingine zitakazobainisha na kueleza majukumu yazo katika mawasiliano ya kimazungumzo. Nadharia nyingine pia zinaweza kutumiwa kupima jinsi fasiri za misimbo hufikiwa katika mazungumzo.

# MAREJELEO


Aitchison, J. (2002) 3rd ed. *Words in the Mind*. U.S.A: Blackwell Publishing.

Arege, T. na Nyanje M. (2011). *Kamusi Fafanuzi ya Methali*. Nairobi : Target Publications.

Bennet, P. (2002). *Semantics: An Introduction to Non-Lexical aspects of Meaning.* Muechen Lincon: GmbH.

Bickmore, L. S. (1998). www.albany.edu/anthro/bickmore.phb. July 5, 2013.

Blommaert, J. (2005) *Discourse: Key Topics in Sociolinguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Chimerah, R. (1998). *Kiswahili, Past, Present and Future Horizons.* Nairobi: Nairobi University Press.

Crystal, D. (2003) *The Cambridge encyclopaedia of English Language, 2nd Edition*. Cambridge: Cambridge University Press.

Dijk, A. Van Teun (2008) *Discourse and Power*. London: Palgrave.

Dusan Stamenkovic (2010). *Meaning Shifts in Interpreting Spatial Bodily Idioms*. http://dx.doi.org/10.2039/ssrn. 1728042 13/05/2013.

Farsi, S. S. (1973). *Swahili Idioms.* Nairobi: East African publishing House.

Finnegan, R. (1977) *Oral literature in Africa*. Oxford: Oxford University Press.

Guthrie, M. (1948). *Classification of Bantu Languages.* London: Dawsons of Pall Mall.

__________ (1970). *Collected Papers on Bantu Linguistics.* England: Gregg International Publishers Ltd.

Habwe, J., Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix.

Kapinga, M. C. (1983) *Sarufi ya Kiswahili Sanifu.* Dar-es salaam: Tuki.

Kapiyo, J., Kiruthu, F., Muma, M. (1996). The Evolving World: A History and *Government Course Form I.* Nairobi: Oxford University Press.

Kiango, J. G (2000) *Bantu Lexicography. A Critical Survey of the Principles and Process of Constructing Dictionary Entries.* Tokyo ILCAA.

Kimani, S. K. (2008). *An Analysis of Truth Conditions in Pragmatic Relevance Theory Approach*. University of Nairobi Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa).

Leech, G. (1983). *Principles of Pragmatics*. London: Longman.

Macdonell, D. (1986) *Theories in Discourse*. Oxford: Basil Blackwell.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., Hokororo J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*. Dar-es-salaam: Tuki.

Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing Co. Ltd.

__________ (1991). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Nairobi : Longman.

Mekacha, R. D. K. (2004). *Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R. (1999) *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longhorn.

Mwebia, F. G. (2006). *A Lexical Pragmatic Analysis of Sense Relations in Kimeru*. University of Nairobi. Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa).

Ngoge, A. T. (2012). *A Relevance Theoretic Analysis of Implications in Ekegusii Idioms – A Case of Communication in Kiobegi Market*. University of Nairobi. Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa).

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ogola, C. A. (2006). *A Pragmatic Analysis of Intercultural Communication Failures*. University of Nairobi. Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa).

Osinde, K. N. (1988). *A Morphophonology of Ekegusii*. University of Nairobi. Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa).

Otiso, Z. K. (2008). *A Morphosyntactic Analysis of Ekegusii Verb Derivations in the Minimalist Programme.* University of Nairobi. Tasnifu ya M. A. (Haijachapishwa).

Ottenheimer, H. J. (2006). *The Anthropology of Language. An Introduction to Linguistic Anthropology*. Canada: Thomson Wadsworth – online

Polome (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington Centre for Applied Linguistics.

Rosch (1975). *Journal of Experimental Psychology General* vol. 104(3).

Sperber, D., Wilson, D. (1986). *Relevance, Communication and Cognition*. Oxford: Blackwell.

Szabo (2006) AIATSIS: URL http://www.anu.edu.au/linguistics/nash/aust/domains/html 04/04/2013.

Thomas, J. (1995). *Meaning in Interaction*. Edinburg: Pearson Education.

Tuki, (2006). *English-Swahili Dictionary, 3rd Edition*. Dar-es-Salaam: Tuki.

Ullman, S. (1970) *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Basil Blackwell.

Voegelin (2006). AIATSIS: URL http://www.anu.edu.au/linguistics/nash/aust/domains/html 04/04/2013.

Wamitila, K. W. (2001). *Kamusi ya Methali*. Nairobi : Sasa Sema.

____________ (2003). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Focus Books.

Wasdensjo, C. (1998). *Interpreting as Interaction.* London: Longman.

Whiteley, W. H. (1965). *A Practical Introduction to Gusii*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Yule, G. (1996). *Pragmatics*. London: Oxford University Press.

# KIAMBATISHO

## HOJAJI

Mimi ninaitwa Alice Kerubo Ochichi. Mimi ni mwanafunzi wa somo la Isimu ya Kiswahili (uzamili) katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Ninafanya utafiti juu ya lugha ya Ekegusii. Naomba uchukue muda wako kuijaza hojaji hii. Toa habari za kweli bila uoga wowote. Usiandike jina lako. Habari zote zitashughulikiwa kama siri.

1. Umri wako (age)
   a) 25 – 30
   b) 31 – 35
   c) 36 – 40
   d) 40 na zaidi
2. Jinsia (gender)
   a) Uume
   b) Uuke
3. Kiwango cha elimu
   a) Elimu ya msingi
   b) Elimu ya sekondari
   c) Elimu ya chuo cha anuwai
   d) Chuo kikuu
   e) Nyingineyo (bainisha)
4. Kazi unayofanya
   i) Mwanafunzi

ii) Umeajiriwa

iii) Umestaafu

iv) Mfanyibiashara

v) Mwalimu

vi) Mkulima

vii) Nyingineyo (bainisha)

Eleza maana za juu juu na maana fiche za kauli zifuatazo

1) Moraa osookire

 i) ____________________

 ii) ____________________

2) Sam n’eriiso erimo

 i) ____________________

 ii) ____________________

3) Enyomba eria yabunirwe

 i) ____________________

 ii) ____________________

4) Kae omwana oyio emete akire

 i) ____________________

 ii) ____________________

5) Mondetere abaachokoro baane mbatwere amate.

i) ______________________________________________

ii) ______________________________________________

6) Omwana bw'Osoro osirire

i) ______________________________________________

ii) ______________________________________________

7) Esese embe n'yangori 'ntaambe

i) ______________________________________________

ii) ______________________________________________

8) Tata omwabo Petero n'eyarare.

i) ______________________________________________

ii) ______________________________________________

9) Abana babeire buna ching'uko

i) ______________________________________________

ii) ______________________________________________

10) Omwana o'bande 'mamiria 'makendu.

i) ______________________________________________

ii) ______________________________________________